SUPA JACKPOT
TZS. 1,090,583,531
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#



UKURASA 3

**SIMULIZI** Simba Bob Junior alivyouawa


KUKITHIRI UVUVI MABOMU... Wavuvi Pwani watoa siri nyuma ya pazia hujuma zao baharini

ama
ALHAMISI MACHI 16, 2023
AFYA NA MAZINGIRA

KIMBUNGA KINATIKISA MSUMBIJI... Wataalamu watoa elimu madhara tabianchi; maradhi, utapiamlo...

Ukurasa 13

Ukurasa 14

Watanzania zaidi 800 katika foleni ya kupandikizwa figo

mazoezi, kuepuka matumizi ya tumbaku na bidhaa zake, kupunguza matumizi ya vilevi na kuzingatia ulaji wa mlo kamili, wenye mbogamboga na matunda ya kutosha, ili kuimarisha kinga ya mwili dhidi ya magonjwa,"anasema.

Waziri Ummy anahimiza kupunguza matumizi ya chumvi, sukari na vyakula vyenye mafuta mengi na kuzingatia unywaji wa maji ya kutosha walau lita 2.5 kwa kila siku, huku kukiwapo uzingatiaji matumizi ya dawa ambazo hazijatolewa maelekezo ya kitaalamu na daktari.

Anaongeza kuwa, takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinabainisha asilimia 10 ya watu wote duniani wanaishi na ugonjwa sugu wa figo na zaidi ni kwa wenye umri zaidi ya miaka 75, wastani wa nusu yao wana tatizo hilo.

Kuhusu utekelezaji Sera ya Afya ya Mwaka 2007 na tatizo figo, Waziri Ummy anasema serikali...

UKURASA 11

Nipashe
Alhamisi Machi 16, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581251
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US

# LAAC yageuka mbogo majibu ya TAMISEMI

UKURASA 2



Katibu wa Taasisi ya Jumuiya na Taasisi za Kiislamu, Shekhe Ponda Issa Ponda akizungumza na waandishi wa habari katika ofisi za Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), Dar es Salaam jana, wakati akiomba serikali kuwaachia huru mashekhe wote wanaotuhumiwa kwa ugaidi. Kulia ni Mkurugenzi Mtendaji wa Kituo hicho, Dk. Anna Henga. **PICHA: SABATO KASIKA**

## LHRC yatoa mapendekezo manne kumaliza mkwamo kesi mashekhe

UKURASA 2

UKURASA WA 4

### DAKTARI BINGWA ADAI MGONJWA ALIKUBALI

DAKTARI Bingwa wa upasuaji magonjwa ya kifua, shingo na tumbo, Maurice Mavura, ameieleza mahakama kuwa Florence Samwel, aliliridhia kufanyiwa upasuaji wa kuondoa tezi la pili la upande wa kulia na pia alielezwa kuwa tezi hilo halikuwa na ugonjwa wa kansa...

## Msafara ACT-Wazalendo wapokewa kwa ndoo tupu za maji

UKURASA 3

UKURASA WA 4

### AFDB, EU, AFD ZAIPA TANZANIA BIL.750/-

TANZANIA imepokea msaada wa Sh. bilioni 750 kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), kwa ajili ya mradi wa umeme wa maji...

UKURASA WA 5

### KAMATI YA BUNGE YARIDHISHWA UJENZI MACHINJIO

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, imeipongeza serikali kwa kufanya uwekezaji wenye tija kwenye machinjio ya kisasa ya Nguru Hills na kuishauri kuhakikisha nyama inayozalishwa inakubalika...



Rais Samia Suluhu Hassan akipokea shada la maua kutoka kwa mtoto, Malaika Adam Issara, baada ya kuwasili jijini Pretoria jana, kwa ajili ya ziara ya kiserikali nchini Afrika Kusini. **PICHA: IKULU**

MICHEZO SIMBA, YANGA ZAKIMBIANA FA UK. 24
KATUNI UK. 6



Mwenyekiti wa Chama cha Kampuni za Gesi nchini, Araman Benoite (kulia), akijadiliana jambo na baadhi ya wadau wa gesi baada ya kufungua kongamano la kimataifa la kampuni za gesi Afrika Mashariki jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# LAAC yawa mbogo majibu ya TAMISEMI

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

KAMATI ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC), imegeuka mbogo kwa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), baada ya kutoa majibu yasiyoridhisha kwenye maazimio 12 ya bunge, huku ikitoa wiki tatu ofisi hiyo ipeleke majibu ya uhalisia.

Miongoni mwa maazimio ambayo yamekosa majibu ni hatua zilizochukuliwa kwa halmashauri 155 zilibainika kushindwa kukusanya marejesho ya Sh. bilioni 47 yanayotokana na mikopo ya vijana, wanawake na watu wenye ulemavu.

Akitoa maelekezo kwa TAMISEMI jana baada ya kukutana kuchambua maazimio yaliyotolewa na Bunge Novemba mwaka jana kutokana na hoja za ukaguzi za mwaka 2020/21, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Halima Mdee, alisema suala la mikopo hiyo limekuwa 'donda ndugu' na Bunge lilieleza mamlaka ya nidhamu ichukue hatua kwa halmashauri zilizobainika kushindwa kukusanya fedha hizo, lakini hadi sasa utekelezaji haujafanyika.

"Fedha zinatolewa mabilioni kwa mwaka mmoja halmashauri zinaweza kutoa kati ya Sh.bilioni 55 hadi 67, changamoto kubwa ni fedha zinatolewa, lakini hakuna marejesho kwa mwaka mmoja halmashauri 155 zimeshindwa kukusanya Sh. bilioni 47 yaani zimetoa mikopo, lakini haijarudi," alisema.

Kuhusu hoja ya upatikanaji wa ruzuku kwenye mamlaka za serikali za mitaa, Mdee alisema ilibainika halmashauri 19 zilipata fedha zaidi ya kiasi kilichopitishwa na bunge huku halmashauri 163 zikipata fedha pungufu, lakini majibu ya TAMISEMI yaliyotolewa hayajaridhisha na kamati hiyo.

Alisema Sh. bilioni 47.1 zimeonekana kutumika zaidi ya bajeti iliyopitishwa na Bunge na ilitakiwa kuelezwa kwanini matumizi hayo yamefanyika.

"Kuna halmashauri zimependelewa zimepata nyingi kuliko ilivyostahili wengine kwa zaidi ya asilimia 50, zingine zimepata pungufu yalivyostahili, lakini kuna halmashauri tatu tu zimepata kama ilivyostahili, sasa tunapopitisha bajeti kuna sheria ya matumizi tunapitisha ambayo tunatoa kibali kwa serikali kutumia kwa kadri tulivyogawa," alisema.

Akizungumzia kuhusu hoja nyingine ya tija katika uwekezaji wa mitaji ya umma ambayo Bunge liliagiza kuandaliwa kwa mwongozo na kanuni kuhusu uwekezaji wa miradi kwenye mamlaka za serikali za mitaa unaozingatia fursa zilizopo.

"Nyie ni mashahidi sasa hivi miradi mingi inafanyika kwenye halmashauri lengo likiwa ni kuchochea kuongeza mapato ya ndani, lakini kumekuwa hakuna mwongozo mahsusi kwa halmashauri husika ili kufanya uwekezaji wenye tija, matokeo yake mabilioni ya shilingi yanatumika kuwekeza kwenye kitu ambacho mwisho wa siku ni white elephant kama Dodoma hapa Soko la Ndugai ukizunguka kuna miradi kama hii kibao," alisema.

Alisema kamati kutokana na hali hiyo ilipendekeza bungeni na kuazimiwa utolewe mwongozo ambao halmashauri zitawekeza kulingana na fursa zilizopo kwenye maeneo yao.

"Kuna hoja watumishi wanadai stahiki zao huko nayo ni kubwa sasa leo kwasababu hazijajibiwa kikamilifu tumeipa serikali wiki tatu ilete majibu ambayo yatawezesha sisi kupendekeza kwa Bunge hatua kali zaidi zichukuliwe ili yeyote aliyepewa dhamana huko chini kuanzia wakurugenzi na wasaidizi wao, waziri mwenye dhamana, sisi tutafanya kazi yetu kwa ufanisi mkubwa."

"Kama walizoea kufanya kazi kwa mazoea hii kamati ina matarajio makubwa ya kufanya makubwa, ili majibu yakija yawe majibu yenye uhalisia na tija, hii dhamana tutatekeleza kwa uadilifu na umakini mkubwa," alisema.

Naye Mjumbe wa kamati hiyo, Ester Bulaya, alisema kwa miaka 10 hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) takribani 700 kwenye halmashauri hazijafanyiwa kazi kwa mujibu wa sheria.

Awali, Naibu Waziri Ofisi ya Rais, TAMISEMI, Dk. Festo Dugange, akitoa majibu ya baadhi ya hoja kwa kamati hiyo, alikiri kuwa hoja ya hatua zilizochukuliwa kwa halmashauri ambazo zimeshindwa kukusanya marejesho ya fedha za mikopo haijajibiwa kikamilifu na kufafanua kuwa tayari wamewasilisha kwa mamlaka ya nidhamu wakurugenzi waliobainika kwenye hoja hiyo.

Aidha, alisema majibu ya maazimio 12 wameandaa majibu, lakini kuna upungufu kamati imebainisha watakwenda kufanyia kazi ili kuwasilisha kwa muda waliopewa.

# LHRC yatoa mapendekezo manne kumaliza mkwamo kesi ya mashekhe

**Na Sabato Kasika**

KITUO cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC), kwa kushirikiana na Taasisi za Jumuiya ya Kiislamu, kimetoa mapendekezo manne kwa serikali ili kumaliza mkwamo wa kesi ya mashekhe waliopo mahabusu katika Gereza la Ukonga jijini Dar es Salaam.

Akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya kituo hicho, Kijitonyama Dar es Salaam jana, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC, Anna Henga, alisema kuna haja kwa serikali kumaliza kesi hiyo.

"Tunapendekeza Mwendesha Mashtaka wa Serikali awafutie mashtaka au awafikishe mahakamani kwa mujibu wa sheria za Tanzania na kuzingatia haki za kikatiba," alisema Anna.

Alisema kwa wiki mbili kumekuwa na mjadala mkubwa unaoendelea katika jamii, mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kuhusu taarifa ya kifo cha Shekhe Said Mohamed Ulatule (80).

"Shekhe huyo aliripotiwa kufariki dunia Machi 4, mwaka huu akiwa mahabusu katika Gereza la Ukonga Dar es Salaam," alisema.

Alisema Mwendesha Mashtaka wa Serikali, katika kifungu cha 91 cha Sheria ya Mwenendo wa Mashauri ya Jinai kama yalivyofanyiwa marejeo mwaka 2022, anaweza kumaliza mkwamo huo.

"Pendekezo letu la pili ni kwamba ufanyike uchunguzi wa kina kuhusu chanzo cha kifo cha Shekhe huyo na utaratibu huo uendelee kwa wote wanaopoteza maisha wakiwa mikononi mwa vyombo vya dola kwa mujibu wa Sheria ya Uchunguzi wa Vifo Sura ya 24 ya mwaka 1980 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2019," alisema.

Katika pendekezo la tatu, Anna anaishauri serikali kuwaachia huru au iwape haki ya kujitetea mahakamani watuhumiwa wote waliokaa gerezani kwa zaidi ya mwaka mmoja bila mashauri yao kusikilizwa.

"Katika pendekezo la nne, tunashauri Haki Jinai inayoendelea na zoezi la kukusanya maoni nchini, itumie fursa hii kupendekeza kwa Rais watuhumiwa wote wa makosa ya ugaidi waliokaa mahabusu kwa zaidi ya mwaka mmoja, ambao baadhi yao wamefikisha miaka 10 bila kesi zao kusikilizwa, Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP), awaachie huru, hasa kwa kuwa viashiria vingi vinaonyesha uwapo wa uonevu badala ya ukweli," alisema.

Katibu wa Taasisi za Jumuiya ya Kiislamu, Shekhe Ponda Issa Ponda, alisema watu wanashikiliwa katika magereza mbalimbali nchini, kwa tuhuma za ugaidi na kushauri sakata hilo limalizwe. "Mambo mengi ya maridhiano yamejikita zaidi kwenye siasa, lakini upande huu ambao leo tunaouzungumzia ni kama umesahaulika," alisema Shekhe Ponda.

Katibu huyo alifafanua kuwa lengo lao sio kuzungumzia walioko magerezani, bali mfumo mzima wa haki za binadamu ili usaidie kuishi kwa amani. Akizungumza na waandishi wa habari makao makuu ya kituo hicho jana, Mkurugenzi Mtendaji wa LHRC Anna Henga, alisema Kuna haja kwa serikali kumaliza kesi hiyo.

"Tunapendekeza Mwendesha Mashtaka wa Serikali awafutie mashtaka au awafikishe mahakamani kwa mujibu wa sheria za Tanzania na kuzingatia haki za kikatiba," alisema Anna.

Alisema kwa wiki mbili kumekuwa na mjadala mkubwa unaoendelea katika jamii, mitandao ya kijamii na vyombo vya habari kuhusu taarifa ya kifo cha Shekhe Ulatule.

## Simulizi simba 'Bob Junior' alivyouawa

**Na Halfani Chusi**

HATIMAYE njama za muda mrefu ya kupoteza utawala wa simba maarufu kama 'Bob Junior', zimefanikiwa baada ya kushambuliwa hadi kufa na kundi la simba wenzake watano katika eneo la mashariki mwa Uwanda wa Namiri katika Hifadhi ya Taifa ya Serengeti (SENAPA).

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Kamishna wa Uhifadhi wa Shirika la Hifadhi za Taifa Tanzania (TANAPA, William Mwakilema, tukio hilo lililotokea hivi karibuni ni la asili kwenye familia za simba kutokana na ushindani unaotokea ili kupata nafasi ya kuongoza kundi.

Jina la 'Bob Junior' lilitokana na wingi wa nywele zake ambazo zilifananishwa na za mwanamuziki maarufu wa muziki wa Reggae nchini Jamaica, Robert Nestor Marley, maarufu kama Bob Marley (sasa marehemu).

"Mapambano kwa familia za simba huanza wanapofikia umri wa miaka mitatu ambao mara nyingi hulazimika kuachana na kundi ili kuanza maisha binafsi mpaka anapopata nafasi ya kushindania uongozi wa kundi.

"Bob Junior alikuwa na umri wa miaka 12 na amekuwa kiongozi wa kundi kwenye eneo hilo kwa kipindi kirefu. Katika kugombea uongozi wa kundi, mara nyingi kiongozi wa awali anashindwa kutetea uongozi wake kutokana na kuwa dhaifu, umri mkubwa au ugonjwa," alisema.

Mwakilema alisema mara nyingi madume yanayoondolewa kwenye uongozi yanakuwa na muda mfupi wa kuishi kutokana na kutengwa kwenye kundi yakiwa na umri mkubwa na wakati mwingine hujeruhiwa wakati wa vita vya kuondolewa au kuuawa wakati wa ushindani.

Pia alisema simba huyo hatafanyiwa mazishi yoyote kwa kuwa kwa kawaida ni asili ya mzunguko wa maisha ya wanyama na kwamba kiikolojia akifa huachwa porini, ili aoze na kuwa chakula cha wanyama wengine.

"Kutokana na kwamba alikuwa porini hadi tunakwenda eneo la tukio, muda ulikuwa umepita hakuna masalia yoyote ya simba huyu yaliyopatikana, hivyo tutakachofanya ni kuandaa historia yake na picha zake kama kumbukumbu katika kituo chetu cha habari," alisisitiza.

**TAARIFA MTANDAONI**

Kwa mujibu wa video fupi iliyosambaa mtandaoni, 'Bob Junior' akiwa kwenye harakati zake, alivamiwa na simba wenzake watatu na kuanza kumrarua sehemu mbalimbali za mwili wake, zikiwamo mgongoni na kwenye maeneo ya shingo mpaka pale umauti ulipomfika.

'Bob Junior' akisaidiana na kaka yake, Joel, walitawala kwa zaidi ya miaka mitano na kuwa miongoni mwa simba waliotawala kwa kipindi kirefu zaidi kabla ya kufikwa na madhila hayo.

Mhifadhi Mwandamizi wa SENAPA, Fredy Shirima, alifafanua tukio hilo ni asilia katika uhifadhi, lakini pia hutokea zaidi kwa simba ambao hushikilia utawala dhidi ya wengine wanaoitaka ngome.

"Bob Junior aliuawa Machi 11, mwaka huu, akishambuliwa na simba watatu ambao walikuwa sehemu ya kundi la simba saba waliokuwa wanapanga mapinduzi. "Hatuwezi kuingilia maisha ya wanyamapori, hivyo kilichotokea kilipangwa miongoni mwao, ikiwa ni vita vya kimapinduzi na simba huwa wana tabia hiyo mtawala anapozeeka hutolewa kimabavu," alisema.

Shirima anaendelea kusimulia kuwa 'Bob Junior' alikuwa na sifa za kipekee kama vile kuwa na manyoya mengi zaidi kuliko simba wengine, lakini mwenye kuvutia kwa mwonekano na hutulia pale anapopigwa picha na watalii. Kifo hicho, kimeibua hali ya simanzi kwa wadau wa wanyamapori na sekta ya utalii kwa ujumla kutokana na tabia alizokuwanazo 'Bob Junior' enzi za uhai wake.



Kiongozi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, akiangalia ndoo walizoshika wanawake waliofika kumpokea Urambo mkoani Tabora jana, wakiashiria tatizo la maji katika eneo hilo. **PICHA: JULIETH MKIRERI**

# Msafara wa ACT - Wazalendo wapokewa na ndoo tupu za maji

**Na Julieth Mkireri,** URAMBO

MSAFARA wa Chama cha ACT - Wazalendo ukiwa katika wilaya ya Urambo mkoani Tabora, umepokewa na wananchi waliokuwa na ndoo tupu za maji, wakiashiria kuomba kusaidiwa kutatua kero hiyo.

Wananchi hao waliokusanyika katika viwanja vya Wananchi Square mjini hapo, walimweleza kiongozi wa chama hicho, Zitto Kabwe, kwamba awasaidie kuwatua ndoo kichwani kutokana na kutumia muda mwingi kutafuta maji.

Kwa mujibu wa Zitto, awali ilielezwa kwamba yatatolewa maji katika Mto Malagarasi Kigoma kwa ajili ya Urambo na Kaliua na pia ilitolewa kauli nyingine kuwa mradi wa maji Ziwa Victoria unaopeleka maji Tabora utafikisha pia Urambo.

"Kwa hiyo nimeshtuka nafika hapa napokewa na ndoo kwamba mradi haujafika Urambo na bado wananchi wana kero ya maji ya miaka yote," alisema Zitto.

Alisema tatizo la maji katika mji wa Urambo ni la muda mrefu na jambo la kushangaza ni kwamba serikali haijalipa uzito kwa kuleta ufumbuzi na wananchi hao kupata maji kupitia miradi inayotekelezwa.

Kutokana na hali hiyo, Zitto alitoa wito kwa Waziri wa Maji, Juma Aweso kushughulikia suala la maji katika mji wa Urambo kwa haraka iwezekanavyo kwa kueleza mradi utakaowanufaisha wananchi hao.

"Namtaka Waziri Aweso aje Urambo aeleze ni mradi gani utatatua tatizo hili la muda mrefu. Atoe taarifa tujue Urambo itafaidika na mradi wa maji wa Ziwa Victoria wa Tabora au mradi wa Malagarasi tufahamu ni mradi upi ambao Urambo utafaidika nao kwenye miradi ya maji.

"Kila wakati tunahamishwa tu sasa Waziri wa Maji awaeleze wananchi ni mradi upi utamaliza tatizo la maji ni aibu sana mji kama huu, wilaya ya zamani hadi sasa haina maji ni jambo ambalo halikubaliki," alisema.

Aliongeza kuwa: "Na sisi tunaahidi tutaendelea kulisemea suala hili kupitia mawaziri wetu vivuli ndani ya chama tumeamua hatuko kwa ajili ya kulalamika, ila tutasimama kushughulikia kero za wananchi kwa kuzifikisha serikalini zipatiwe ufumbuzi."

Pia alisema Waziri wa Kilimo anatakiwa kulitolea ufafanuzi kwa haraka suala la mbolea ambalo baadhi ya wakulima walinunua mbolea kwa dola mara mbili ya bei elekezi ya serikali.

Aliwataka wakulima walionunua mbolea watunze risiti, ili uandaliwe mkakati wa kuitaka serikali kurejesha fedha hizo ambazo walilipia mbolea tofauti na bei elekezi.

"Hiyo mbolea ya ruzuku kwanza ilichelewa wakulima wakachelewa kupata lakini pia sehemu ya mbolea hiyo ikachukuliwa na watu wachache wakauza kwa dola, mbolea ambayo ingeuzwa kwa Sh. 60,000, au 59,000 ikauzwa kwa dola 59 ambayo ni zaidi ya Sh.100,000 suala hili limeniumiza sana," alisema.

Alisema tayari amemweleza Waziri wa Kilimo ashughulike na suala hilo na wakuwa utakusanya nakala za risiti na tutaziwasilisha serikali wakulima wote walionunua mbolea kwa dola, ili kukomesha suala hilo kutokea tena.

Kiongozi huyo alisema chama hicho kimeunda mfumo wa mawaziri vivuli kwa ajili ya kufikisha kero kwa serikali ili ziweze kushughulikiwa.

Awali, Philbert Macheyeki, ambaye ni Waziri Kivuli wa Mawasiliano, Teknolojia, Habari na Uchukuzi, alisema kwa muda mrefu zao la tumbaku halijawanufaisha wakulima tangu uhuru, lakini kwa msimu huu mbolea haijawafikia wakulima walio wengi na hata waliopata imechelewa kuwafikia.

Pia alisema maji yamekuwa kikwazo hali inayosababisha wanawake kutumia muda mwingi kwenda kutafuta huduma hiyo na kusimamisha shughuli nyingine za maendeleo.

Akizungumzia kuhusiana na suala hilo kwa njia ya simu Waziri wa Maji, Aweso alisema tayari serikali imesaini mkataba kwa ajili ya kusambaza maji kutoka Ziwa Victoria na kati ya maeneo yatakayonufaika ni pamoja na Urambo na Kaliua.


EAST AFRICAN CRUDE OIL PIPELINE

BBN Limited TZA

**OMBI LA KUONESHA MASLAHI YA UGAVI WA VIFAA VYA KUPIMIA KAZI ZA KUCHOMELEA, KUPAKA, MEP NA ZEGE**

**KUMBUKUMBU Na: ETJ-BB-PR-EI-GEN-GE-0116**

Jamhuri ya Uganda, Kampuni ya Taifa ya Mafuta ya Uganda (UNOC), Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na/au Shirika la Maendeleo ya Petroli Tanzania (TPDC), pamoja na makampuni mengine ya kimataifa ya mafuta yanashiriki katika utekelezaji wa Mradi wa EACOP.

Uendelezaji wa Mradi wa EACOP unahusisha uhandisi, ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bomba la kusafirisha mafuta ghafi linalovuka Uganda na Tanzania ikijumuisha Gati yenye Kituo cha Kupakia Mafuta kwenye Meli za Mafuta, karibu na Tanga nchini Tanzania.

BESIX Ballast Nedam Limited, inayotekeleza Huduma za Awali za Ujenzi wa Gati na Kituo cha Kupakilia katika Ghuba ya Tanga kwa ajili ya Mradi wa Bomba la Mafuta Ghafi la Afrika Mashariki (EACOP), inakaribisha Makampuni ya kitaalamu kueleza nia yao kwa Ugavi wa:

- **Vifaa vya kupimia kazi za kulehemu (Kuchomelea), Upakaji rangi maalumu, MEP na Zege.**

**MAELEZO MAFUPI YA WIGO WA VIFAA /HUDUMA:**

Vifaa vya kupima vinaweza kutofautiana kwa kila kazi kama vile;

***Kazi za kulehemu:*** Vipimo vya kulehemu, vifaa vya NDT (MPI, PT, PAUT, RT), vifaa vya kudhibiti joto na nk.

***Kazi za Kupaka:*** WFT, DFT, Holiday Test, Pull-off test, Kipimo cha Vumbi (Dust Test) na nk. ***Kazi za MEP:*** Vipimo vya shinikizo, kinasa sauti cha hydrotest, vifaa vya kudhibiti halijoto, multimeters , kipima ardhi cha ardhini, mita ya kubana, kipimo cha voltage , kijaribu kebo na n.k.

***Kazi za Zege:*** Vipima joto, uchunguzi wa halijoto ( Testo au sawa), vifaa vya kupima saruji safi (slump, kiwango cha hewa, jotoridi), vifaa vya kupima maabara cha kokoto, mchanga, saruji nk.

**KIWANGO CHA MAHITAJI:**

Kampuni zinazoonyesha nia yao zinaalikwa kuandika ombi lao kwa kuonyesha:

- Wasifu wa kampuni wenye uthibitisho wa uwezo wa kutosha wa kifedha na rasilimali za kutosha na zenye uwezo.
- Orodha ya kina ya vifaa husika vya upimaji na karatasi ya data (datasheet) muhimu
- Kuzingatia kanuni za mafuta ya petroli ya matumizi ya rasilimali za ndani (Local Content) ya 2017 na ufafanuzi wa kampuni ya ndani kwa Tanzania.
- Uthibitisho wa usajili/maombi kwa hifadhidata ya Watoa Huduma kwa Wasambazaji wa Ndani (LSSP) wakati wa kuwasilisha jibu kwa usemi huu wa maslahi unapendekezwa sana.

Makampuni yanayovutiwa ambayo yanakidhi mahitaji ya chini kabisa na yana uwezo wa kutoa huduma zilizoorodheshwa hapo juu wanapaswa kueleza nia yao kwa kutuma barua pepe pamoja na hati zilizoorodheshwa hapo juu kwa **procurement@bbnltd.co.tz (Ukubwa wa Barua Pepe na viambatanishi MB 20 & Nyaraka zote lazima ziwasilishwe kwa lugha ya Kiingereza) mnamo au kabla ya tarehe 31 Machi 2023 , Saa 12 jioni kwa saa za Tanzania,**

Makampuni yanayokidhi kwa kuridhisha mahitaji ya chini kabisa yaliyo hapo juu yatatathminiwa na yakichaguliwa yataalikwa, kulingana na saini ya Makubaliano ya Kutofichua (NDA), ili kushiriki katika mchakato wa zabuni.

**Kumbuka:** Kampuni zilizohitimu awali pekee ndizo zitapokea mwaliko wa kuwasilisha zabuni yao ili kuendeleza mchakato wa Wito wa Zabuni.

# Daktari Bingwa adai mgonjwa alikubali kupasuliwa

**Na Grace Gurisha**

DAKTARI Bingwa wa upasuaji magonjwa ya kifua, shingo na tumbo, Maurice Mavura, ameieleza mahakama kuwa Florence Samwel, aliliridhia kufanyiwa upasuaji wa kuondoa tezi la pili la upande wa kulia na pia alielezwa kuwa tezi hilo halikuwa na ugonjwa wa kansa.

Florence alifungua kesi ya madai katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam akidai fidia ya Sh. milioni 500 dhidi ya Hospitali ya TMJ na Hindu Mandal zote za jijini Dar es Salaam pamoja na Dk. Mavura kwa madai kuwa alifanyiwa upasuaji ambao utamfanya anywe dawa maisha yake yote.

Hayo yalielezwa jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Ramadhani Rugemalila, wa mahakama hiyo wakati akitoa ushahidi wake dhidi ya kesi iliyofunguliwa na mdai kwa sababu yeye ndiye daktari ambaye alimfanyia upasuaji huo Florence na kusababisha aweze kupumua vizuri.

Akiongozwa na wakili wake, Ngassa Mboje, Dk. Mavura alidai kuwa mgonjwa (Florence) alikubali kufanyiwa upasuaji wa pili ili hatua ya tatu ya matibabu ya dawa ya kunywa ya mionzi uanze.

"Florence baada ya kufanyiwa upasuaji wa mara ya pili ya kuondoa tezi la upande wa kulia katika Hospitali ya Hindu Mandal, kinyama cha uvimbe kilipelekwa Hospitali ya TMJ kwa ajili ya kupima kansa, lakini majibu yaliporudi yalionesha hana kansa," alidai Dk. Mavura.

Alidai kuwa taarifa hiyo alimweleza mgonjwa (Florence), na kumwelekeza aende katika Taasisi ya Saratani ya Ocean Road kwa ajili ya kuanza matibabu ya dawa ya mionzi ya kunywa kwa ajili ya homoni kwa sababu tayari mdai alishatolewa tezi mbili.

Pia alidai mahakamani hapo kuwa kama mgonjwa hata fanya hatua ya tatu ya matibabu, tatizo litakalompata ni ugonjwa huo (kansa) utaota sehemu ile ile au sehemu nyingine ambayo ni kuanzia shingoni, kifuani na hata kwenye mapafu.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Aprili 18, 2023 kwa ajili ya Dk. Mavura kuendelea kutoa ushahidi wake sambamba na vielelezo ikiwamo nyaraka ambayo inaonesha mgonjwa aliliridhia kufanyiwa upasuaji wa mara ya pili kwa kusaini.

Awali, aidai mwaka 2018 alimfahamu Florence kutokana na tatizo alilokuwa nalo la tezi kushuka hadi eneo la kifua na kusababisha ashindwe kupumua vizuri na baada ya kuzunguka kwa madaktari wengi wa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (MNH) bila majibu alielekezwa amuone yeye.

Dk. Mavura alidai Juni 27, 2018, Florence alienda katika Hospitali ya Muhimbili na alipofanyiwa uchunguzi kwa kupimwa vipimo mbalimbali ambavyo vilionesha tatizo lake ambalo mtaalamu wa kushughulikia tatizo hilo alikuwa ni yeye.

Alidai kuwa Julai 7, 2018 alionana na Florence katika Hospitali ya Hindu Mandal, alimfanyia vipimo na alibaini alikuwa na tatizo kwenye njia ya hewa iliyosababishwa na tezi ya kushoto kuvimba na kuelekea kifuani.

"Nilimweleza Florence tatizo lake na wakati tunazungumza alikubali kufanyiwa upasuaji kwa kuliondoa tezi hilo ili aweze kupumua vizuri kutokana na kwamba uvimbe huo ulisababisha yeye kutokupumua vizuri," alidai Dk. Mavura.

Aliendelea kudai kuwa tezi zipo mbili, lakini aliiondoa moja ya upande wa kushoto kwa sababu ndiyo iliyoonekana inashida kutokana na vipimo alivyopimwa.



Meneja wa miradi vituo vya kupoza umeme kwa miradi ya Zambia, Tanzania na Kenya (ZTK), Timothy Mgaya, akitoa maelezo ya mradi wa ujenzi wa kituo cha umeme mkubwa wa kilovoti 400 cha Tagamenda mkoani Iringa kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) walipotembelea mradi huo juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# AfDB, EU, AFD zaipa Tanzania bil.750/-

**Na Gwamaka Alipipi**

TANZANIA imepokea msaada wa Sh. bilioni 750 kutoka Benki ya Maendeleo Afrika (AfDB), Umoja wa Ulaya (EU) na Shirika la Maendeleo la Ufaransa (AFD), kwa ajili ya mradi wa umeme wa maji wa Kakono mkoani Kagera.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini Dar es Salaam, baada ya kutia saini mkataba wa kupokea fedha hizo, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, alisema lengo kuu la mradi huo ni kuongeza uzalishaji wa nishati kwenye gridi ya taifa.

Alisema lengo lingine ni kukabiliana na upungufu wa umeme katika maeneo ya Kaskazini-Magharibi mwa Tanzania.

Dk. Nchemba alisema kukamilika kwa mradi huo kutaondoa matumizi ya gharama kubwa ya mitambo ya dizeli ya kuzalisha umeme Kaskazini-Magharibi, katika Kanda ya Ziwa na kuepuka kukatika na kupunguza mgawo wa umeme kwa kanda hiyo.

Alisema mradi huo utakamilika ndani ya miaka mitano kuanzia sasa, utahusisha ujenzi wa mtambo wa kufua umeme wa megawati 87.8.

Pia alisema mradi huo pia unahusisha usambazaji wa umeme na utekelezaji wa mpango wa usimamizi wa mazingira na kijamii.

Dk. Nchemba alisema Kanda ya Ziwa ni eneo lenye tija kubwa katika uzalishaji wa madini na samaki wanaouzwa nje, kwamba uhitaji wa nishati ya umeme kwa gharama nafuu na wa uhakika ni jambo la msingi kwa ustawi wa sekta husika.

Alisema kwa zaidi ya muongo mmoja sasa, Kanda ya Ziwa imekuwa na sifa ya matumizi ya mitambo ya kutumia nishati ya dizeli na ya gharama kubwa na kutokuwa na umeme wa uhakika na wa kutosha.

"Katika kutatua tatizo hilo serikali iliomba AfDB na AFD kufadhili mradi wa umeme wa maji wa Kakono. Kwa pamoja - AfDB; AFD kwa ushirikiano na EU na serikali ya Tanzania zimekubali kufadhili mradi huu wenye thamani ya Dola za Marekani milioni 325 sawa na Sh. bilioni 750," alisema.

Meneja Mkazi wa AfDB Tanzania, Patricia Laverley, alisema mradi wa Kakono utaongeza uzalishaji na kupunguza mgawo wa umeme, kuimarisha uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya wananchi.

Mkurugenzi Mkazi wa AFD Tanzania, Céline Robert, alisema kutiwa saini kwa mkataba huo kutaimarisha utendaji kazi wa serikali kufikia malengo ya mwaka 2025 katika sekta ya nishati.

Mkuu wa Ushirikiano wa EU, Cedric Merel, alisema Sh. bilioni 86.7 walizozitoa zitaimarisha na kuboresha upatikanaji wa nishati jadidifu.

# Kamati yaridhishwa maandalizi utekelezaji mradi wa umeme

**Na Mwandishi Wetu**

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), imeeleza kuridhishwa na maboresho ya kituo cha kupokea, kupooza na kusafirisha umeme mkubwa cha Tagamenda mkoani Iringa, ili kuongeza upatikanaji wa nishati hiyo.

Mradi huo unajulikana kama "Backbone Transmission Investment Project (BTIP)" awamu ya pili utakaosafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga yenye urefu wa kilomita 670.

Akizungumza wakati wa ziara hiyo, Makamu Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Japhet Hasunga alisema lengo la ziara hiyo ni kujiridhisha na utekelezaji wa mradi huo unaolenga kuviongezea uwezo vituo vya kupokea na kupoza umeme mkubwa katika mikoa ya Iringa, Singida, Dodoma na Shinyanga kutoka umeme mkubwa wa kilovati 220 kwenda mkubwa wa 400.

"Tumejiridhisha na maendeleo yake tumejionea mradi ulishaanza kutekelezwa na nguzo zilishasimikwa na vyuma vimeshasimikwa kila mahali na vimekamilika na tayari sasa wanaanza kujenga ile 'substation' kubwa ambayo itapokea kilovoti 400 kwa hiyo tulikuwa tunajiridhisha ni sehemu gani umeme wa kilovoti 400 itajengwa na tumeshajionea na tumeona, lakini pia nyuma yetu tumeona kwamba kuna umeme ambao ni kilovoti 220 ambao tayari umeshakamilika" alisema Hasunga ambaye pia ni Mbunge wa Vwawa.

Naye Mkurugenzi Mtendaji wa Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Maharage Chande, alisema mradi wa Backbone Transmission Investment Project (BTIP) umekamilika kwa awamu ya kwanza iliyohusu ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme mkubwa wa kilovoti 400 kutoka Iringa hadi Shinyanga na upanuzi wa vituo vya kupokea na kupoza umeme mkubwa wa kilovoti 220 kwenye mikoa ya Iringa, Dodoma, Singida na Shinyanga na kwamba kituo kinapokea umeme kutoka katika mabwawa ya Kidatu, Kihansi na Mtera.

"Mradi huu umekamilika kwa awamu ya kwanza kwa maana ya kituo cha kilovoti 220 na kinapokea sasa umeme kutoka katika vituo vya kuzalisha umeme kwa maji vya Mtera, Kidatu, na Kihansi. Kituo hiki kina manufaa makubwa ya kuwezesha nchi yetu kuwa na umeme wa uhakika na wenye ubora, kikikamilika kitaweza kupeleka umeme kwenye zaidi ya mikoa 18 ambayo sasa hivi inapata umeme kutoka kwenye kituo hiki," alisema.

Aidha, aliongeza kuwa mradi huo wa upanuzi utakapokamilika utawezesha kupeleka umeme katika nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) ambako kuna fursa kubwa ya kuuza umeme.

"Lakini vilevile kituo hiki ni cha kupeleka umeme katika nchi za "Southern African Power Pool (SAPP)" kupitia nchi ya Zambia ambapo kwa sasa hivi kuna fursa kubwa za kuuza umeme kwa sababu kwa upande huo umepungua, lakini pia kuunganisha nchi za upande wa Mashariki "Eastern African Power Pool (EAPP)" kupitia nchi za Kenya, Uganda na Ethiopia.

"Mradi huu unategemewa kuanza kutekelezwa hivi karibuni kwani tupo katika hatua za manunuzi, tunategemea mpaka mwezi wa nne au wa tano zitakuwa zimeshamilika na kuanza kupata mkandarasi wa kuanza kujenga kituo hiki cha upanuzi na njia kuu za kupeleka katika kituo kinachofuata cha Kisada, na Iganjo, ili umeme uweze kusafiri na kuweza kufika ," alibainisha Chande.

## HABARI KITAIFA



Washiriki wa mkutano wa maofisa watendaji wakuu (CEO's) wakifuatilia mada zilizokuwa zikitolewa kwenye mkutano ulioandaliwa na Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), jijini Dar es Salaam jana, kwa ajili ya kubadilishana mawazo kuhusu kozi zinazotolewa na chuo hicho. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Majaliwa aahidi kusomesha watoto wawili wa mwandishi aliyefariki

**Na Said Hamdani,** LINDI

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, ameahidi kuwasomesha watoto wawili wa mwandishi wa habari wa Kituo cha Channel Ten, marehemu Abdullaziz Ahmadi, kwa kuwasomesha hadi watakapohitimu masomo yao.

Alitoa ahadi hiyo jana mkoani hapo, alipokuwa anatoa salamu za pole kwa wafiwa, wakati wa mazishi ya mwandishi huyo yaliyofanyika makaburi ya Bomolea.

Mwandishi wa Habari Chanel Ten ameacha mke mmoja na watoto wawili, Ahmad Abdullaziz anayesoma Shule ya Sekondari ya Nyangao iliyopo Halmashauri ya Mtama na Sheda Abdullaziz anayesoma Shule ya Msingi Mary Majaliwa, Kata ya Chimbira, Wilaya ya Ruangwa mkoani humo.

Alisema kutokana na uhusiano mzuri kati yake na mwandishi huyo wakati wa uhai wake atabeba jukumu la kusomesha watoto hao ili wafikie ndoto zao.

Alisema wakati wa uhai wake, mwandishi huyo amewahi kushika nyadhifa mbalimbali zikiwamo za siasa kama Mjumbe wa Kamati Kuu ya Taifa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) ngazi ya wilaya na klabu ya waandishi wa habari mkoa wa Lindi (LRPC).

Awali, baba mdogo wa marehemu, Mohamedi Abdullaziz, akizungumza kwa niaba ya ukoo, alimshukuru Waziri Mkuu kwa ushirikiano aliowapa wakati kijana wao amelazwa Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.

"Kwa niaba ya familia, nachukua nafasi hii kukushukuru Waziri Mkuu kwa kazi kubwa uliyoifanya, ikiwamo kushiriki gharama za matibabu za kijana wetu," alisema.

Aidha, Mohamedi ambaye amewahi kuwa Mbunge wa Jimbo la Lindi Mjini kwa miaka 15 pamoja na mkuu wa mkoa wa Tanga na Iringa, alisema familia imepokea kwa moyo wa shukrani msaada huo.

# DC mstaafu afagilia utendaji Rais Samia

**Na Elizabeth Zaya**

MKUU wa Wilaya ya Bahi mstaafu, Elizabeth Mkwassa amesema katika kipindi cha miaka miwili cha uongozi wa Rais Samia Suluhu Hassan, amewarejesha wafanyabiashara waliofunga biashara zao baada ya mifumo ya kuwaumiza katika miaka kadhaa iliyopita.

Akizungumza na Nipashe jana, Mkwassa alisema kabla ya kuingia madarakani Rais Samia, wafanyabiashara wengi walikata tamaa na kufunga biashara zao kwa kile alichodai walikuwa wakikandamizwa na kikosi maalumu kilichojulikana kama 'TRA Task Force'.

"Rais Samia katika kipindi hiki cha miaka miwili, amefanya nchi imetulia zaidi, nazungumza hili kwa sababu mimi ni mfanyabiashara, miaka michache iliyopita, sisi wafanyabiashara tulikuwa na shida sana hasa kwenye upande wa masuala ya kodi, tumepata shida sana na baadhi ya viwanda vilirudi nyuma kwa sababu hiyo na hata wafanyabiashara wengine waliamua kufunga biashara zao," alisema Mkwassa.

"Kulikuwa na kitu kinaitwa 'TRA Task Force' hii ilitusumbua mno, wakati mwingine ulikuwa unajikuta unadaiwa fedha hata ambayo huijui na ilikuwa ni vigumu kubisha, hii ilituumiza sana, lakini tangu ameingia mama (Rais Samia), kwanza fedha zetu ambazo tulitozwa isivyo sahihi zilirudishwa.

"Kwa kweli katika suala hilo la kuiweka vizuri TRA ni kitu kikubwa ambacho nitaendelea kumkubali na ninamuombea kwa Mungu aendelee kufanya makubwa, na sasa hivi tunaongea nao kama marafiki, wanakufundisha mpaka muelewane na tunalipa kodi bila matatizo, kwa sasa mtu unajisikia vibaya kutolipa kwa sababu tuko nao vizuri."

Alisema wafanyabiashara wengi walikata tamaa na hivyo kuona hakuna haja ya kuendelea kufanya biashara.

"Unajua hakuna kitu kibaya kama kukatishwa tamaa, TRA mwanzoni walikuwa wanatukatisha tamaa sana, watu waliona kwa nini wafanye biashara wakati fedha zikipatikana wanachukua wao, bora uache. Kwa hiyo watu wengi waliacha na wengine walikimbia hata nchi wakaenda zao huko, katika hilo tunamkubali sana Rais Samia."

Alisema Rais Samia amevunja mwiko uliokuwa unaaminika na tamaduni nyingi za kiafrika kwamba nafasi ya urais ni ya wanaume pekee.

"Nimpongeze Rais Samia. Unajua kwenye tamaduni hizi za kiafrika unapokuwa kiongozi mwanamke ni lazima ufanye kazi mara mbili, kuwaongoza wanawake na wanaume hasa kwa sababu tamaduni zetu ziliaminisha watu kuwa baadhi ya kazi ni za wanaume, lakini Rais Samia katika hilo amepambana na amevunja huo mwiko," alisema.Alisema katika kipindi cha miaka miwili ya uongozi wake, Rais Samia amefanya nchi imetulia zaidi.

"Tulikuwa tumezoea kwamba mwanamume ndiye anayeweza nafasi ya urais, lakini tunaona mama ameweza na amefanya mambo makubwa zaidi ambayo hayajawahi kufanyika, kwa hiyo tushikamane, tupendane na tuendelee kumtia moyo, tushikamane na mama yetu aendeleze kazi njema aliyoianza ili tuandike historia."

# Kamati ya Bunge yaridhishwa ujenzi machinjio

**Na Halfani Chusi**

KAMATI ya kudumu ya Bunge ya Ustawi na Maendeleo ya Jamii, imeipongeza serikali kwa kufanya uwekezaji wenye tija kwenye machinjio ya kisasa ya Nguru Hills na kuishauri kuhakikisha nyama inayozalishwa inakubalika kimataifa, ili kupata soko la uhakika ndani na nje ya nchi.

Pongezi hizo zilitolewa jana na wajumbe mbalimbali wa kamati hiyo, walipotembelea machinjio hayo yaliyopo Mvomero, mkoani Morogoro.

Mwenyekiti wa Kamati hiyo, Fatma Tawfiq baada ya kutembelea machinjio hayo, alipongeza kazi nzuri iliyofanywa na serikali huku akishauri uboreshaji huo ufanyike kwenye machinjio mengine.

"Hongereni sana tumeona kazi hii nzuri, uwekezaji ni mzuri sana tunawapongeza na pongezi za pekee kwa Rais Samia Suluhu Hassan, kwa juhudi zake kubwa, tunamwombea nia yake njema kwa taifa letu ifanikiwe kwani uwekezaji huu ni matokeo ya sera nzuri za serikali yetu," alisema.

Pia aliwataka wajumbe wa kamati hiyo kuhakikisha wanaishauri serikali na wawekezaji wengine kiwanda hicho kithibitishwe kimataifa, ili bidhaa zake ziweze kuuzwa katika soko lolote ulimwenguni.

Naye Mjumbe wa kamati hiyo ya Bunge, Kabula Shitobelo, alisema, "Hongereni sana kiwanda ni kizuri sana tumekitembelea na tumeona jinsi kinavyofanya kazi."

Mjumbe mwingine, Sophia Mwakagenda, pamoja na kuridhishwa na uwekezaji huo ambao umeshatoa ajira kwa vijana 300, alishauri kuwekwe usimamizi mzuri ili kiwanda kiwe na tija kwa taifa.

Alisema mradi huo unakwenda kuwa mkombozi mkubwa kwa wafugaji na wajasiriamali akisisitiza kama wakiutumia vizuri utawasaidia kuongeza kipato chao pamoja na pato la nchi.

Mjumbe mwingine, Neema Mwandabila, alisema katika kuhakikisha nyama ya Nguru inawafikia Watanzania wengi kiwanda kimejipanga kufungua maduka katika maeneo mbalimbali ili kila Mtanzania aweze kunufaika.

Akijibu baadhi ya hoja za wajumbe wa kamati hiyo, Mkurugenzi Mkuu wa PSSSF, Hosea Kashimba, alisema katika kuhakikisha nyama ya nguru inawafikia Watanzania wengi kiwanda kina mpango wa kufungua maduka katika maeneo mbalimbali na kwa kuanzia duka limeshafunguliwa Morogoro mjini.


## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA/NOTISI

**TANFIN CONSULTANT E.A LTD** Kwa niaba ya **BUNJU BEACH/SELFPROJECT SACCOS LTD.** Tunatoa notisi na Tangazo la mnada kwa Mdaiwa wao anaesomekahapa chini awe amelipa deni lake analodaiwa na **SACCOS** hiyo kinyume na hapo tutauza dhamana na mali yake kwa njia ya mnada wa hadhara. Mnada utafanyika sehemu dhamana/mali husika ilipo na tarehe kama inavyotangazwa hapo chini

| S/N | JINA LA MDAIWA | AINA YA DHAMANA NA MAHALI ILIPO | TAREHE NA MUDA WA MNADA |
|---|---|---|---|
| 1. | SALUM SAID SEIF | NYUMBA ILIOPO MTAA WA KILUNGULE, KATA YA BUNJU, WILAYA YA KINONDONI, BLOCK 9 PLOT NAMBA 113. | 7/04/2023, MUDA: SAA 5: 00 ASUBUHI NA KUENDELEA. |

**MASHARTI YA MNADA**

1. Mnada utafanyika sehemu dhamana ilipo na zitauzwa kama zilivyo.
2. Mnunuzi atakayeshinda atalazimika kulipa asilimia ishirini na tano (25%) ya bei iliyofikiwa papo hapo na asilimia sabini na tano (75%) italipwa ndani ya siku 14 kuanzia tarehe ya mnada. Endapo mteja atashindwa kumalizia 75% ndani ya siku 14 kiasi kilicholipwa awali cha 25% hakitarudishwa na mnada utarudiwa tena.
3. Gharama za kubadilisha umiliki **(TRANSFER OF OWNERSHIP)** pamoja na gharama nyingine zinazohusiana na umiliki wa mali hizi ni juu ya mnunuzi.

**Mobile: 0785 944 141, 0699222677**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Serikali isitishe uamuzi wa kufuta bima Toto Afya Kadi

**KATIKA** wiki hii, kumekuwa na mjadala mzito kuhusu uamuzi wa Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kuweka masharti mapya ya bima ya afya kwa watoto kwa kusitisha 'Toto Afya Kadi'. Badala yake, mfuko huo umetaka wazazi kuwasajili watoto hao kama wategemezi kupitia vifurushi vya bima vinavyotolewa na taasisi hiyo.

Kutokana na uamuzi huo, wadau mbalimbali, wakiwamo wanachama wa bima ya afya, wameibuka na kutoa maoni yao huku wengi wakionyesha kutoridhishwa na jambo hilo. Wameeleza kwa uwazi kwamba hatua hiyo itasababisha matatizo makubwa katika upatikanaji wa bima ya afya hususan kwa watu wa kipato cha chini.

Wadau hao hawakuishia hapo tu bali wameiomba serikali kuangalia upya uamuzi huo na kwamba maboresho ya sekta ya afya yazingatie makundi maalum katika jamii, hususan watoto.

Wakati wananchi wakilalamikia mfumo mpya kwa matibabu ya bima ya afya kwa watoto, NHIF imefafanua kuwa uamuzi wake huo umetokana na utafiti uliofanyika na kuonyesha kuwa kuna ongezeko la kipato katika sekta isiyo rasmi baada ya serikali kurasimisha maeneo mengi hali iliyosababisha Watanzania wengi kumudu gharama za bima.

Hoja kubwa inayotolewa na NHIF kama uthibitisho wa jambo hilo ni kwamba Watanzania wengi wana simu za mkononi ambazo wamekuwa wakizitumia kwa mawasiliano na kwamba idadi kubwa wana uwezo wa kununua bando la Sh. 2,000. Kwa mantiki hiyo, kutokana na watu hao kumudu kununua mabando ya simu, ni dhahiri kwamba wana uwezo wa kumudu gharama za bima ya afya.

Aidha, NHIF katika kujibu hoja zilizotolewa na wadau ilibainisha kwamba uamuzi wa kufuta Afya Toto Kadi utasaidia kupanua wigo wa wanachama na kwamba utafiti unaonyesha kuwa watoto wenye umri wa miaka 18 ni asilimia 31 ya Watanzania wote.

Kama kilivyosema Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu (LHRC) ambao ni wadau wa masuala mtambuka yanayohusiana na haki za binadamu, afya ikiwamo, katika taarifa yake juzi, utaratibu wa bima ya afya ya Toto Afya Kadi umekuwa msaada kwa mamilioni ya watoto wa kitanzania. Utaratibu huo, ni dhahiri kwamba ulikuwa mkombozi kwa watoto wengi wasio na uwezo wa kumudu gharama za matibabu na ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakisaidiwa na wasamaria wema.


Ni lazima serikali ikatambua kwamba sehemu kubwa ya Watanzania ni wale wanaotafuta riziki kwa ajili ya kujikimu kimaisha na hawana uwezo kama ilivyodai NHIF kupitia utafiti wake kwamba wana uwezo wa kununua bando la vocha ya simu!

Utafiti wa kuzingatia kigezo kimoja hautoi majibu kuhusu jambo fulani bali ungeangalia vigezo vingine. NHIF katika utafiti wake, tunadhani, ingeangalia pia taarifa za Ofisi ya Taifa ya Takwimu kuhusu hali ya kipato katika kaya badala ya kuja na hoja ambayo haina mashiko.

Kuibuliwa kwa jambo hili kumewasha moto ambao unaweza kusababisha majanga kwa Watanzania, kwa maana ya wananchi wengi kushindwa kumudu gharama za matibabu kwa sababu ya uwezo wao kiuchumi.

Matokeo ya moja kwa moja hayawezi kuonekana sasa bali siku zijazo na umakini usipozingatiwa, kuna hatari kubwa ya wengi kupoteza maisha kwa kushindwa kumudu gharama za matibabu. Ni vyema suala hili likaangaliwa upya badala ya kila upande kuwa na mtazamo wake sawa na msemo wa mwamba ngoma ngozi huvutia kwake.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Uchafuzi wa mtoni hadi Ziwa Victoria Mwanza, hatua iliyoko ni hatari zaidi

Na Anthony Gervas, MWANZA

**JIJI** la Mwanza ni kubwa na hadi sasa linashika nafasi ya pili kwa idadi ya watu Tanzania. Sensa ya Watu na Makazi inatuambia wako milioni 3.669, likitanguliwa na Dar es Salaam. Mandhari yake Mwanza, imezungukwa na milima, mabonde, Ziwa Victoria kwa upande wa Magharibi mwa jiji. inapendeza kwelikweli!

Hapo kuna vivutio vingi kuanzia kwa wakazi wake na wageni wanaofika mahali hapo kufanya shughuli mbalimbali, zikiwamo biashara na utalii, pasipo kusahau hifadhi ya kisiwa cha Saanane.

Niseme, kama ilivyo chochote kwa asili yake, kizuri hakikosi kasoro. Nako jijini Mwanza ni hivyo hivyo! Kuna kinachopigwa vita kitaifa na kimataifa, ni kero ya kuchafua mazingira.

Katika Mto Mirongo, uliopo jijini humo, ambao ni maarufu na unaungana na Ziwa Victoria, maji yake na taka mbalimbali hukusanywa na mto na kuingizwa ziwani.

Kwanza naamini sote tunaungana na uhalisia huo kwamba, ni kinyume na kanuni za mazingira, afya, matunzo ardhi, maji, utalii na mengi tu. Sasa ndio hapo najiuliza, mamlaka za usafi wa mazingira na idara za afya, zimepotea wapi kuondoa aibu na kero hizi jamani?

Au bado tunabaki kukumbatia utamaduni wa kusukumwa, ndio viongozi wa kiserikali na watendaji wao wakurupuke kuanza kuwajibika na hilo?

Wageni kutoka nje ya jiji la Mwanza na nchi jirani, hufika kujionea mandhari haya ya jiji hilo na vivutio vyake, wakiwamo samaki wa kila aina na biashara.

Ukifika hata leo penye Mto Mirongo na hasa mvua zikiwa zinanyesha, utashuhudia na kushangaa taka ngumu za plastiki, mifuko na chupa za maji, zikisombwa na maji kupitia mto huo.

Hivi sasa mto ni mchafu kuliko kawaida. Maji na taka zimesambaa kuelekea ziwani bila ya udhibiti wa namna yoyote. Sijui, wenye dhamana wanasubiri kusukumwa na nani, ndio wachukue hatua stahiki kusimamika usafi huo wa kimazingira?

Tukumbuke maji yanayoingia Ziwa Victoria kupitia Mto Mirongo, hutumiwa na wananchi wa mikoa mbalimbali Kanda ya Ziwa, kunywa binadamu, mifugo na wanyama wengineo.

Kutokana na huduma za maji hayo, huenda zikageuka kuwa changamoto, watu na viumbe hai wengine kuathirika afya zao wakipata magonjwa yasiyoambukiza yatokanayo na maji. Vilevile kuna maji hayo kuwa na sumu zitokanazo na taka hizo.

Mamlaka husika zimeshindwa kusimamia na kudhibiti hatari hii ya uchafuzi wa mazingira, kulinda afya za watu wanaotumia huduma ya maji ya Ziwa Victoria wakiwamo maelfu ya wavuvi, ambao wengi wawapo visiwani, huchota na kuyatumia moja kwa moja bila ya maboresho yoyote kiafya.

Ndugu zangu wa Baraza la Taifa la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), hili haliwahusu? Au nanyi mnasubiri mpaka madhara yatokee, ndio hekaheka zianze? Tuambieni katika utafiti wenu Ziwa Victoria, hadi sasa limeathirika kiasi gani na taka zinazoingia humo?

Nirejee kwa wenyeji serikali mtaa, kwanini sheria ndogo hazitiliwi mkazo kuhakikisha zinatumika kwa wananchi wanaokiuka namna ya kuhudumia taka? Kuanzia Meya na Mkurugenzi Jiji, madiwani na wabunge hamna pa kulikwepa hili?

Hapo pia panahusu barabarani, ambako hakuna usimamizi wa kutosha au wasimamizi mnataka hadi taka hizo zitupigie hodi milangoni mwa ofisi, ndiyo mchukue hatua?

Inashangaza sana, unaweza ukadhani kuna uhalisia wa msemo 'baba akisafiri watoto hujitawala.' Jiji letu maarufu Mwanza liwe safi kuanza na Mto Mirongo, tukisogea hadi mitaroni na miferejini, ambako taka zimesambaa.

Niweke wazi kuna upungufu katika hatua za kukabili usafi Mwanza kuanzia katika mbinu za kuhakikisha mito inabaki salama, hali kadhalika ziwa lenyewe. Ni wakati wa kujitathmini na kuchukua hatua.

Niwasogezee jicho langu kuanza na vyanzo vya wachafuzi mazingira mitaani; wafanyabiashara na machinga wanaokaidi kanuni za afya.

Ziwa Victoria hili ndilo linalohudumia maji katika Mradi wa Maji ya Ziwa Victoria, yakifikisha kwa mikoa kadhaa sasa, hivyo una heshima kubwa kitaifa na kimataifa. Viongozi na watendaji wa Jiji Mwanza, sijui mna tafakari ya hilo?

HABARI KITAIFA




Meneja Mwandamizi wa Biashara wa Benki ya Azania, Jackson Lohay, akitoa mada katika kongamano la Siku ya Wanawake Wajasiriamali Afrika lililoandaliwa na Chama cha Wafanyabiashara Wanawake Tanzania (TWCC) Dar es Salaam wiki iliyopita ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Mwanamke Duniani. Benki ya Azania ilidhamini mkutano huo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wadaiwa kumuua mama warithi mali

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

JESHI la Polisi mkoani Njombe linawashikilia watu wanne kwa tuhuma za kumuua kwa kumnyonga mama yao mzazi, Fatuma Kimbawala (80) mkazi wa mtaa wa Magongo mjini Makambako, kwa kile kilichodaiwa kutaka kurithi mali.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Hamis Issah, alisema tukio hilo lilitokea Machi 13, mwaka huu, majira ya saa 7:00 mchana.

"Bado kuna masuala ya kuwania mali, kugombea mali za urithi bado halijaeleweka katika jamii tofauti tofauti. Mkoa wa Njombe hakikisheni kama kuna mali inagombewa au kuna mali inatakiwa kufanyiwa ufafanuzi nani apewe, nani asipewe, kuna vyombo mbalimbali ambavyo mnaweza kutumia," alisema.

"Wazee wa mila wanaweza kutumika, mahakama inaweza kutumika na wale wazee wa mila hakikisheni mnapoamua maamuzi yasilete utata. Sehemu zingine zikipata sintofahamu na kubaki na kisa matokeo yake yanakuja madhara kama haya, si kumuondoa mtu ambaye anaitunza, ili ninyi mgawane. Kwa hiyo sasa hivi hata hiyo mali hamtagawana kutokana na mambo mliyoyafanya," alisisitiza.

Katika hatua nyingine, Polisi wanamshikilia Medrad Mbigi (28) mkazi wa mtaa wa Mpechi mjini Njombe, kwa tuhuma za kumnajisi mtoto wa kambo mwenye umri wa miaka minane, mwanafunzi wa darasa la kwanza, kwa kile kilichoelezwa ni kuondoa mikosi kwenye biashara zake na kujipatia utajiri.

Kamanda Issah alisema: "Huyu baba amekuwa anambaka mtoto wa kufikia wa mke wake ambaye anakaa naye, hili jambo linahusisha mambo yanayohusiana na ushirikina na tunachofanya sasa hivi kule ambako ushirikina umeanzia ndiko tutakuwa tunafuatilia mpaka kuona huyu aliyesababisha anakamatwa."

Aidha, alitoa rai kwa wakazi wa mkoa wa Njombe kwamba pindi unapoona mtoto anakulalamikia juu ya vitendo vya ukatili watoe taarifa polisi.

"Endapo unaona ewe mzazi wa kike au wa kiume tafadhali sana tunawaomba na tunawataka mtoe taarifa kituo cha polisi kwa ajili ya hatua ambazo zinatakiwa na sio vinginevyo kwa sababu ukiona baba na mama mnakaa halafu mtoto anaathirika kutokana na matukio ya kunyanyaswa ama matukio ya kubakwa ama kulawitiwa,mama upo baba upo.

"Hili jambo tuliangalie sana wanandugu majirani tunaomba msaidie kutoa taarifa hapa inaonekana kweli kuna mambo kuhusiana na ushirikina kama kuna mambo yanayohusiana na ushirikina Njombe tuache mambo hayo yatatufikisha mahali ambako ni pabaya," alisema.

Kamanda Issah alisema jeshi la polisi litawachukulia hatua kali watakaobainika kuendeleza vitendo vya unyanyasaji watoto kwa imani potofu.

"Hili jambo halikubaliki na ni kinyume cha sheria za nchi yetu ya Tanzania," alisema.

Akizungumza na Nipashe, Mwenyekiti wa Mtaa wa Mpechi, Enesmo Kilasi, alisema alipata taarifa kwenye mtaa wake kwamba kuna mtu anabaka mtoto wake.

"Nilipopata taarifa kwa sababu ya taratibu zetu nilianza kwanza kwa balozi wake ili kupata taarifa za ndani zaidi na kweli balozi alitoa ushirikiano mkubwa, aliniletea mtu ambaye anaishi naye pale nyumbani ili kabla sijachukuwa hatua zaidi nijiridhishe, hapa amefika takribani miezi miwili kwa hiyo yule mtoto alikuwa akiumwa tumbo na maradhi mengine, yule baba alianza kumuingilia mtoto kwa muda mrefu," alisema Kilasi.

# Mrakibu polisi kortini madai wizi 600,000/-

**Na Grace Gurisha**

MRAKIBU Msaidizi wa Polisi (ASP), Lydia Ngua na wenzake wanne, wamepandishwa kizimbani katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam wakikabiliwa na shtaka la wizi wa Sh. 600,000.

Washtakiwa wengine ni Shaban Hamis, Shukuru Mwagu, Mpelembe Mpelembe na Thaa Mwagu, wote wakazi wa Dar es Salaam.

Akisoma ya mashtaka, Wakili wa Serikali Caroline Matemu, mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Amir Msumi wa mahakama hiyo alidai kuwa washtakiwa wanatuhumiwa kwa kosa moja la wizi.

Matemu alidai Februari 21, 2022 washtakiwa wote kwa pamoja wakiwa eneo la Charambe Kisutu, Wilaya ya Ilala, Dar es Salaam, waliiba Sh. 600,000 mali ya Sophia Mbaga.

Matemu alidai upelelezi wa kesi hiyo umekamilika na kuiomba mahakama kupanga tarehe nyingine ya kuwasomea washtakiwa hoja za awali.

Washitakiwa wote walikana mashtaka yao na wameachiwa kwa dhamana baada ya kukamilisha masharti ya dhamana ya kuwa na mdhamini mmoja aliye saini bondi ya Shiling milioni moja.

Kesi hiyo iliahirishwa hadi Machi 23, 2023 kwa ajili washtakiwa kusomewa maelezo ya awali.

**KABWELA** Na Fadhili Mohammed



# Serikali, wadau waandaa muundo wa nishati safi

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

SERIKALI kwa kushirikiana na wadau wengine wa sekta ya nishati nchini, imeanza kuandaa muundo wa Mfuko maalum wa nishati safi ya kupikia.

Pia inaandaa dira na mkakati wa miaka 10 ya kuhamia kwenye nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka huu.

Hatua hiyo inalenga kutekeleza agizo la Rais Samia Suluhu Hassan alilolitoa Novemba mwaka jana wakati akifungua Kongamano la Kitaifa kuhusu Nishati hiyo lililofanyika katika ukumbi wa Julius Nyerere (JNICC) Jijini Dar es Salaam.

Hayo yalisemwa juzi jijini hapa na Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, wakati akifungua Warsha ya Kitaifa ya siku mbili ya wadau wa nishati safi ya kupikia.

Hafla hiyo iliandaliwa na Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP) na Mfuko wa Umoja wa Mataifa wa Maendeleo ya Mtaji (kupitia Mpango wa Cook-Fund unaofadhiliwa na EU) kwa ushirikiano wa karibu na Wizara ya Nishati, Chama cha Nishati Mbadala Tanzania (TAREA) na Chama cha Wadau wa Nishati Safi ya Kupikia Tanzania (TACCS) na Ofisi ya Makamu wa Rais, Idara ya Mazingira.

Warsha hiyo pamoja na mambo mengine, inalenga kuwaleta pamoja wadau wakuu wa sekta hiyo kutoka serikalini, sekta binafsi na mashirika ya kiraia ikilenga kujadili namna wanavyoweza kutekeleza lengo la kitaifa la kufikisha asilimia 80 ya idadi ya watu wanaotumia nishati safi ya kupikia ifikapo 2033.

Hafla hiyo ilileta pamoja wajasiriamali wa teknolojia ya nishati safi ya kupikia, taasisi za utafiti, mashirika ya kijamii, mashirika ya Umoja wa Mataifa, taasisi za kifedha, mashirika ya ndani na kimataifa, taasisi za serikali na wadau wengine muhimu katika sekta ya nishati.

Akizungumza katika warsha hiyo, Mhandisi Mramba alisema wizara yake kwa kushirikiana na wadau wengine imejipanga kikamilifu kutekeleza maagizo ya Rais Samia kuhusu dhamira ya nchi ya kuendeleza ajenda ya nishati safi ya kupikia.

Katika kongamano la Kitaifa la Nishati Safi ya Kupikia, lililofanyika Dar es Salaam Novemba, mwaka jana, Rais Samia Suluhu Hassan aliiomba wizara hiyo na wadau husika kuandaa mpango madhubuti utakaosaidia kuchochea mabadiliko ya asilimia 80 ya watu katika kupikia nishati safi ifikapo mwaka huu.

Kwa mujibu wa Mhandisi Mramba, tayari serikali imeunda timu maalum ya kitaifa ya nishati safi ya kupikia inayoratibiwa na Ofisi ya Waziri Mkuu ambayo inahakikisha kwamba maagizo yote yaliyotolewa na Rais yanatekelezwa.

"Wizara ya Nishati inaongoza maandalizi yote ya muundo wa mfuko huo kuelekea kufanikisha adhmina hiyo ndani ya miaka 10 kulingana na agizo la Mheshimiwa Rais...niwafahamishe tu kwamba hasi kufikia sasa tunakwenda vizuri," alisisitiza.

Akizungumza katika warsha hiyo Meneja Mpango wa Cook-Fund wa UNCDF, Imanuel Muro, alisema shirika lake kupitia mpango huo unaofadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) linaunga mkono juhudi za Rais Samia.

"Tunazingatia juhudi za pamoja za kuhamia kwenye nishati safi ya kupikia ifikapo mwaka 2023 na ndiyo maana tumekuwa tukitoa ruzuku kwa sekta binafsi, ili sekta hii iweze kuwasaidia watumiaji wa mwisho wa bidhaa hizo waweze kumudu gharama za vifaa vya nishati safi ya kupikia kwa kuwa vitapatikana kwa bei nafuu," alisema. .

Mkurugenzi na Mwakilishi wa WFP, Sarah Gordon-Gibson, alisema: "Mwaka huu WFP inapanga kusaidia karibu nusu milioni ya Watanzania wanaoishi katika mazingira magumu pamoja na wakimbizi wa Burundi na Congo kupitia mipango mbalimbali. kwa kuwa watu wengi tunaowahudumia wanategemea kuni na mkaa kupikia."

Kwa mujibu wa Sarah, upatikanaji wa nishati safi ya kupikia na teknolojia imekuwa ni changamoto kubwa na inayoleta athari mbaya za kiafya, jinsia, kiuchumi, mazingira na hali ya hewa.

Kwa hivyo, alibainisha hatua za pamoja zilizoratibiwa na za kina na juhudi mpya zitahitajika, ikiwa taifa linadhamiria kumaliza changamoto hiyo.




Katibu Mkuu wa Wizara ya Nishati, Mhandisi Felchesmi Mramba, akizungumza na wadau mbalimbali wa nishati safi ya kupikia walioshiriki warsha ya kitaifa ya siku mbili ya nishati safi ya kupikia, jijini Dodoma juzi. Wengine ni Mkurugenzi na Mwakilishi wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Sarah Gordon-Gibson (wa pili kulia) na Meneja Mpango wa CookFund wa Shirika la Umoja wa Mataifa la Maendeleo ya Mitaji (UNCDF), Imanuel Muro (kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Ndugu watiwa hatiani kwa shambulio la mwili

**Na Grace Gurisha**

MKAZI wa Kongowe, Singbard Buchard na ndugu zake wawili, wametiwa hatiani kwa kosa la kumshambulia na kumdhuru mwili Rashid Mohamed na Anitha Rauyan, wanaodaiwa kuchapwa na fimbo na kufungwa mikono na kupelekwa kwa kiongozi wa eneo hilo wakiwashutumu kwa ugoni.

Ilidaiwa kwamba, waliwavamia kwa madai kwamba Mohamed alikuwa anatembea na Anitha ambaye alikuwa mke wa Singbard.

Hakimu Mkazi Mkuu, Evodia Kyaruzi wa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam aliwataja washtakiwa wengine waliotiwa hatiani kuwa ni Albert Buchard na Delfina Bouchard.

Akisoma hukumu hiyo, Hakimu Kyaruzi alisema washtakiwa walikuwa wakikabiliwa na mashtaka mawili ambayo ni shambulio la kudhuru mwili na kusababisha majeraha ya hatari na shtaka la pili ni la kudhuru mwili.

Hakimu Kyaruzi alisema baada ya kupitia ushahidi uliowasilishwa, mahakama imewakuta washtakiwa na hatia kwa shtaka la pili la shambulio la kudhuru mwili.

"Mahakama imeridhika kwamba washtakiwa wote ndiyo chanzo cha walalamikaji kujeruhiwa na hivyo wanatiwa hatiani," alisema Hakimu Kyaruzi.

Alisema washtakiwa wote ni ndugu, walifika eneo la tukio na walihusika kuwashambulia walalamikaji na wote walionekana kuwa na nia moja, waliwavamia na kuwapiga, ushahidi huo unaungwa mkono na matabibu waliyopewa.

Alisema washtakiwa hao wanadaiwa kutenda makosa hayo Julai 29, 2021 eneo la Voda, Kongowe, Wilaya ya Temeke, Dar es Salaam na mahakama inatarajia leo kuwasomea adhabu yao.

Ilidaiwa kwamba, Mohamed na Anitha ni wapenzi na siku ya tukio, washtakiwa waliwavamia wakiwa chumbani.

Aidha, waliwavamia kwa madai Mohamed alikuwa anatembea na Anitha ambaye alikuwa mke wa Singbard. Ilidaiwa kuwa baada ya uvamizi huo, washtakiwa hao waliwapiga Mohamed na Anitha sehemu mbalimbali za mwili kwa kutumia fimbo, waliwafunga mikono na kisha kuwapeleka kwa kiongozi wa eneo hilo wakiwatuhumu kwa ugoni.

Hata hivyo, washtakiwa hao walikana kuhusika kuwadhuru Mohamed na Anitha, huku wakikiri kufika eneo la tukio.

# JICA yarejesha utaratibu wafanyakazi wa kujitolea

**Na Christina Mwakangale**

SHIRIKA la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA), limesema limerejesha utaratibu wa wafanyakazi kupitia mpango wa kujitolea wa ushirikiano wa Japan (JOCV) baada ya kusitisha miaka mitatu kutokana UVIKO-19.

Muda mfupi kabla ya UVIKO-19 mwaka 2020, jumla ya wafanyakazi wa kujitolea 60 wa JICA wa nyanja mbalimbali nchini, walitakiwa kurejea kwao, mara moja.

Februari 7, mwaka huu, mfanyakazi mmoja wa kujitolea anaenda kupangiwa moja ya vituo vya kazi Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) katika fani ya uhandisi wa mitambo.

Taarifa kwa vyombo vya habari kutoka shirika hilo, jana, ilisema kuwasili kwa mfanyakazi huyo, kunaashiria kuanza tena kwa programu ya kujitolea nchini.

"Kwa sasa mfanyakazi wa kujitolea anafanya mafunzo ya lugha ya kiswahili na utamaduni kwa mwezi mmoja kabla ya kuanza kazi yake katikati ya Machi 2023.

Taarifa hiyo, ilisema kwamba, Mjapan huyo anaishukuru Serikali ya Tanzania kwa kukubali kufanya kazi ya kubadilishana maarifa na ujuzi wake na Watanzania.

"Wafanyakazi wa kujitolea wa Japani hukaa Tanzania kwa miaka miwili kufanya kazi katika nyanja mbalimbali zinazochangia maendeleo ya rasilimali watu katika nyanja mbalimbali zikiwamo elimu, utawala bora, afya, TEHAMA, kilimo, mazingira, utalii na michezo."

Mpango wa JOCV ni mojawapo ya Mipango ya ushirikiano wa kiufundi wa Japani inayoendeshwa kama sehemu ya Misaada Rasmi ya Maendeleo (ODA) inayotolewa kusaidi nchi na majimbo yapatayo 98 ikiwa ni pamoja na Tanzania.

Pia, lengo kuu ni kushirikiana katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kubadilishana maarifa na utaalamu wa kiufundi wa Japan katika nchi zinazoendelea na kuimarisha urafiki.

Taarifa, ilibainisha kwamba mpango wa JOCV nchini una historia ndefu tangu mwaka 1966, na hadi sasa JICA imeleta takribani Wajapan 1,700 wa kujitolea kwenye taasisi mbalimbali ili kukabiliana na changamoto za maendeleo.





## RC aziagiza halmashauri kutoa ushirikiano kwa vyama vya siasa

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

MKUU wa Mkoa Arusha, John Mongella, ameziagiza halmashauri za mkoa huo hadi ngazi ya mkoa, kuhakikisha zinatoa ushirikiano kwa vyama vya siasa vya upinzani kama Rais Samia Suluhu Hassan anavyosisitiza suala la maridhiano.

Alitoa agizo hilo jana jijini Arusha katika kikao cha kamati ya ushauri ya mkoa, ambacho kilienda sambamba na uzinduzi wa kitabu cha miaka miwili ya mafanikio ya Rais Samia Suluhu Hassan.

Alisema suala la maridhiano ni la kila mmoja na halipaswi kuachiwa ngazi za juu pekee kwani haitakuwa na maana.

"Nawaagiza ngazi zote kwenye halmashauri hadi mkoa kila mmoja ashirikiane na hawa wenzetu ili kwa pamoja tusonge mbele,"alisema.

Alisema watakapowashirikisha itasaidia kupata mawazo mbadala na kuboresha pale wanapotakiwa kuboreshwa.

Kuhusu kitabu, Mongella, alisema Machi 19 mwaka 2021, Rais Samia atatimiza miaka miwili tangu aingie madarakani, akaona kama mkoa waadhimishe kwa kutoa kitabu kinachoelezea kazi zilizofanywa mkoani humo.

"Lakini tunashukuru kila mmoja kutuwezesha kuwa na uhuru na usalama na kutuwezesha Mkoa wa Arusha kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 533 sawa na asilimia 107.13 katika kipindi cha miaka miwili na lengo la mwaka huu ni kukusanya zaidi ya Sh. bilioni 411," alisema.

Alisema miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia Hassan Suluhu ameboresha sekta ya afya ikiwamo kuboresha hospitali za Wilaya ya Monduli, Longido, Karatu na Ngorongoro, ili wananchi wapate huduma bora za afya, ikiwamo kupunguza vifo vya kinamama na watoto.

Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Mkoa Arusha, Zelothe Steven alisema Rais Samia amefanya kazi nzuri ambayo hawajawahi kuiona.

Alisema tangu aingie madarakani miradi mikubwa iliyokua inatekelezwa na mtangulizi wake hakuna hata mmoja uliozorota.

# CHADEMA yajitosa kutafuta suluhu mgogoro wa ardhi

**Na Mwandishi Wetu,**
ARUMERU

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimejitosa kutafuta suluhu ya mgogoro wa kugomea mgawanyo wa ekari 500 za ardhi iliyotolewa na serikali kwa wakazi wa Kijiji cha Kwa Ugoro, Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha.

Wananchi hao wanapinga serikali kuwalazimisha kulipa Sh. milioni moja kwa ajili ya kupata ardhi hiyo kwa ekari moja na Sh. 500,000 ya kupata ardhi kwa nusu ekari katika Shamba la Valeska lililofutiwa hati na Rais.

Akizungumza jana na wananchi wa Kwa Ugoro, Mwenyekiti wa CHADEMA, Mkoa wa Arusha, Elisa Mungure, alisema wanalaani kinachoendelea katika shamba hilo na wanaitaka serikali kwenda kuwasikiliza wananchi wa kijiji hicho.

Alisema: "Namwomba Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Anjelina Mabula, aje hapa (Kwa Ugoro) kuwasikiliza ninyi 'direct' (moja kwa moja).

Halmashauri imeshaanza kuuza viwanja na kuweka utaratibu mipango ya matumizi bora ya ardhi, lakini ardhi iliyogawanywa kwa vijiji vitatu kikiwamo cha Kwa Ugoro, ndiko kuna sarakasi za kuwatoza fedha wananchi wanunue ardhi, wakati walipewa mgao wa ekari 500.

Aliongeza: "Haikubaliki wananchi kuondolewa kwenye ardhi yao, wakati wana diwani waliyemchagua, wakati kuna Mwenyekiti wa Halmashauri, ambaye anatakiwa awatetee wananchi. Wakati kuna mbunge ambaye kazi yake anatakiwa aseme hiyo shughuli isimame haki itendeke, lakini wako kimya.

Zaidi alisema: "Waziri hawezi kuja hapa bila mbunge, Rais hawezi kuja hapa bila mbunge au bila halmashauri. Sasa hivi eti imefikia mahali watu wa Kwa Ugoro mnafukuzwa kwenye maeneo yenu mlioyojenga. Binadamu kama ninyi ni vikao vikalike mtoe kero zenu, serikali iwasikilize mwambiwe ondokeni kwa utaratibu.

Mwenyekiti wa CHADEMA, Arumeru Mashariki, Gadiel Mwanda, alisema wananchi wa Kwa Ugoro walikuwa na uhaba wa ardhi ya kilimo na ufugaji kwa muda mrefu na wao ndiyo waliopiga kelele wakiomba kupewa ardhi katika Shamba la Valeska lililokuwa likimilikiwa na Chama Kikuu cha Ushirika cha Arusha (ACU), lakini leo wao wanaotaabika.

Shamba hilo la ekari 4,087 linazungukwa na vijiji vya Maroroni, Kwa Ugoro na Valeska, baada ya serikali kufuta umiliki wake kutoka ACU kutokana na kushindwa kuliendeleza, serikali iliagiza kila kijiji kupewa ekari 500.

Mmoja wa wakazi wa Kwa Ugoro, Eliafoo Eliafoo, alisema wananchi wa Kwa Ugoro wanatengenezewa umaskini wakati siyo asili yao.

"Watoto wetu hawaendi shuleni, watoto waliobahatika kwenda shule wanasinzia darasani, ni kwa sababu tumekosa cha kupelela shuleni (chakula). Kwa uhakika ili apate rekodi ya mahudhurio ya watoto shuleni, ndio watakapopata uhakika ni nini tunacholilia,"alisema.

Mkazi mwingine Mary Mollel alisema: "Tunaomba mama aje atutetee (Rais Samia Suluhu Hassan), Waziri aje aone kinachofanyika (Anjelina Mabula). Mtendaji na diwani wetu wana orodha ya wananchi wanodaiwa chakula shuleni, hili shamba hili ndiyo lilikuwa linatunza shule zote.

Leo wanapokea pesa za wananchi na kuwauzia matajiri."



Mwenyekiti wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Wilaya ya Simanjiro mkoani Manyara, Kiria Ormemei Laizer (kulia), akikabidhi moja ya mifuko 100 ya saruji kati ya 200 kwa Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Saniniu Laizer, Swedefrida Msoma, aliyoahidi kwa ajili ya kujengea bweni la shule hiyo katika Kitongoji cha Namelock, Kijiji cha Naepo, Kata ya Naisinyai juzi. **PICHA: WOINDE SHIZZA**

# Wakulima wapewa mbegu zinazohimili mabadiliko tabianchi

**Na Cynthia Mwilolezi,**
ARUSHA

WAKULIMA wa mboga wamepatiwa mbegu mpya ambazo zinauwezo wa kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Mbegu hizo zilitolewa jana na wasambazaji wa mbegu zaidi ya 500 nchini wakati wa mafunzo kwa wakulima (Shamba darasa).

Mafunzo hayo yaliyoandaliwa na taasisi ya usambazaji mbegu ya Balton Tanzania yenye makao makuu yake jijini Arusha.

Akizungumza katika mafunzo hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa Wafanyabiashara wa Mbegu Tanzania (TASTA), Bob Shuma, aliwataka wakulima kujifunza matumizi ya mbegu bora ili kuongeza uzalishaji, kwani serikali imesaidia kuboresha mazingira ya upatikanaji mbegu kwa wakati.

Alisema mbegu bora ambazo zinazalishwa na Balton Tanzania na taasisi nyingine zikitumiwa vizuri Tanzania itakuwa na uwezo wa kuongeza uzalishaji wa chakula na hata kuuza nje.

Mkurugenzi Mkuu wa Kampuni ya Balton Tanzania na Rwanda, Chris Keeping, alisema kama wakulima nchini wakipata mbegu bora wataongeza uzalishaji wa chakula na hivyo kuuza mazao yao nje.


Alisema kwa Tanzania kilimo kinaongoza kwa kuchangia asilimia 30 katika pato la taifa, ambapo zaidi ya asilimia 80 ya Watanzania wanategemea kilimo.

"Leo tunazindua mbegu bora za nyanya, vitunguu, pilipili hoho, kabeji, tikiti maji na mboga ili wakulima wazitumie mbegu hizo kuongeza uzalishaji wa mazao mbalimbali na kuweza kuuza mazao nje ya nchi," alisema.

Meneja wa Balton Tanzania, Ravi Periyasamy, alisema taasisi hiyo itaendelea kutoa mafunzo kwa wakulima na wasambazaji mbegu nchini, ili kuongeza uzalishaji wa chakula.

Periyasamy alisema mbegu mpya ambazo zimeanza kusambazwa na taasisi hiyo zinazingatia athari za mabadiliko ya tabianchi.

Baadhi ya wakulima na wazalishaji wa mbegu walieleza kushuka kwa uzalishaji wa chakula kulikosababishwa na mabadiliko ya tabianchi.



HABARI KANDA YA ZIWA

# RC aagiza ujenzi vituo vya mabasi kuondoa msongamano

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MKUU wa Mkoa Kagera, Albert Chalamila, ameitaka Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba mkoani Kagera kuweka kipaumbele katika ujenzi wa vituo vya mabasi ili kuondoa msongamano wa magari, kuongeza mapato.

Alitoa agizo hilo juzi wakati wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo inayoendelea katika manispaa hiyo ikiwamo Kituo cha Mabasi Kyakairabwa ambacho hadi sasa Sh. bilioni 1.8 zimetolewa kwa ajili ya ujenzi.

Chalamila alisema licha ya halmashauri kuendelea na ujenzi kituo hicho bado wanayo nafasi ya kuweka nguvu katika ujenzi wa vituo vidogo kwa ajili ya kuondoa msongamano wa magari sambamba na kuongeza vyanzo vya mapato katika halmashauri hiyo.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba, Hamid Njovu, alisema mchakato wa ujenzi wa stendi ya mabasi eneo la Kyakailabwa ulianza mwaka 2015 na tayari kimegharimu Sh. milioni 835.

Kadharika alisema katika ujenzi huo imewekwa miundombinu ya barabara kiwango cha changarawe, vituo vya abiria, sehemu ya maegesho yenye ukubwa wa ekari 14.

Aliongea kuwa stendi hiyo ikikamilika itaweza kubeba magari 26 ambayo yataegeshwa wakati wa kutoa huduma ya usafirishaji kwa wananchi.



Ofisa Msimamizi wa Kodi kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) mkoa maalumu wa kikodi Kahama, Godfrey Chama, akitoa elimu ya kodi kwa wafanyabiashara wakubwa na wa kati wilayani Kahama, mkoani Shinyanga juzi. **PICHA: SHABAN NJIA**

# Imani potofu, uhaba vituo wakwamisha utoaji chanjo corona

**Na Alex Say,** MASWA

WAKAZI 120,000 katika Halmashauri ya Wilaya ya Maswa mkoani Simiyu hawajapata chanjo ya ugonjwa wa corona kuliko sababishwa na uhaba wa vituo vya kutolea chanjo hiyo pamoja na imani potofu juu ya chanjo hiyo.

Inaelezwa kuwa chanjo hiyo iliyoanza kutolewa katika Wilaya ya Maswa Agosti 21, 2021 kati ya wananchi 341,324 ni 221,324 ambao wamepata chanjo hiyo.

Hayo yamesemwa juzi na Ofisa Afya na Mratibu wa Huduma ya chanjo Wilaya ya Maswa, Abel Machibya, wakati wa semina ya kutathmini vikwazo vilivyosababisha kushindwa kuwafikia wakazi wote wilayani humo.

Machibya alisema chanjo hiyo haikufanikiwa kuwafikia wakazi wote wa Maswa kutokana na uhaba wa vituo vya kutolea chonjo hiyo.

Alisema awali vituo vya kutolea huduma hiyo vilikuwa ni vinne, kati ya vituo 51 vya kutolea huduma ya afya wilayani humo na halmashauri ina hospitali moja, vituo vya afya vinne na zahanati 46.

"Lengo lilikuwa ni kuwafikia wananchi 221,324 sawa na asilimia 102.03 ya lengo lililowekwa na serikali la kuchanja wakazi zaidi ya 216,000 sawa na asilimia 60 ya jumla ya wakazi wote wilayani," alisema.

Akitolea ufafanuzi juu ya vikwazo dhidi ya chanjo hiyo kwa wakazi wilayani humo, Ofisa Afya wa Wilaya ya Maswa na Mratibu wa Usafi wa Mazingira, Budodi Walwa, alisema mbali na uhaba wa vituo, kauli mbiu ya kitaifa ya kuchanja kwa hiari pia ilichangia baadhi ya watu kuisusia.

"Baadhi yao walitilia mashaka ubora wa chanjo hizo, lakini kulikuwa na tetesi ya baadhi ya wananchi wenye kundi sifuri la damu kudai hawawezi kuchanja kwa kuwa kinga zao zipo imara na isitoshe utoaji wa chanjo ulitolewa kwa kubagua baadhi ya makundi ikiwamo makundi ya vijana walio chini ya miaka 18,"alisema.

Ofisa Utawala kutoka Mtandao wa Radio za Kijamii (TADIO), Fatuma Mahendeka, alisema mtandao huo kwa ufadhili wa Shirika la Internews wanaendelea kuhamasisha utolewaji wa chanjo kwa wananchi wilayani humo, ili kuhakikisha jamii hiyo inafikiwa na chanjo.

## Wapewa elimu kudhibiti utakatishaji fedha na ukwepaji kodi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) umetoa elimu ya namna ya kudhibiti vitendo vya utakatishaji fedha, kukwepa kodi, ugaidi kwa vyombo vya uchunguzi mkoani hapo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kaimu Mkurugenzi wa BRELA, Merdad Rweyemamu, alisema vyombo vilivyopewa elimu hiyo ni vile vilivyoidhinishwa na sheria katika upatikanaji wa taarifa za wamiliki manufaa wa kampuni.

Alivitaja vyombo hivyo ni Ofisi ya Upelelezi wa Makosa ya Jinai, Jeshi la Uhamiaji, Ofisi ya Mwendesha Mashtaka pamoja na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA).

Alisema ili vyombo hivyo viweze kufanya shughuli zake za kiuchunguzi vinahitaji kuelewa namna ya kampuni zinavyotakiwa kufanya kazi, ili kuweza kudhibiti mianya ya utakatishaji fedha.

"Vyombo hivi vimepewa mamlaka ya kisheria ya kupata taarifa kwa ajili ya uchunguzi na uendeshaji wa mashtaka ya jinai yanayohusu kampuni, hivyo kufanya kampuni kuongeza uwajibikaji na uwazi katika shughuli zake," alisema.

Aidha, alisema hatua hiyo inakuja kufuatia takwa la kimataifa la kuhakikisha elimu inatolewa juu ya dhana ya wamiliki manufaa katika kampuni kwa mamlaka zilizokasimiwa.

Mrakibu Msaidizi wa Jeshi la Uhamiaji mkoani Mwanza, Alfredy Mwenda, alisema mafunzo hayo yatawawezesha kutambua wamiliki halisi wa kampuni wenye hisa pamoja, kutambua uraia pamoja na vibali vya kuishi na kufanya biashara nchini.

Ofisa Uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Dorothea Kinyonto, alisema: "Tunafuatilia mali za watuhumiwa pamoja na utakatishaji fedha katika kampuni fulani, hivyo itatusaidia katika uchunguzi wetu unaohusu ukwepaji kodi kwa kuwafahamu wamiliki halisi wanaonufaika na kampuni."

ama
ALHAMISI MACHI 16, 2023
AFYA NA MAZINGIRA



**KIMBUNGA KINATIKISA MSUMBIJI... Wataalamu watoa elimu madhara tabianchi; maradhi, utapiamlo...**

Ukurasa 13



**KUKITHIRI UVUVI MABOMU... Wavuvi Pwani watoa siri nyuma ya pazia hujuma zao baharini**

Ukurasa 14

# Watanzania zaidi 800 katika foleni ya kupandikizwa figo



Wataalamu wa afya kutoka Hospitali ya Rufaa ya Kanda Bugando, wakitoa huduma kwa wananchi waliojitokeza kufanya uchunguzi wa magonjwa ya figo, wiki iliyopita. **PICHA: MTANDAO.**

**Na Yasmine Protace**

UGONJWA wa figo unatajwa kuwa wa hatari na hata kuchangia baadhi ya vifo, kwa wanaochelewa kupata matibabu.

Pia, ugonjwa huo unawafanya watu kutumia gharama kubwa kwa ajili ya matibabu.

Ni Shida inayochangiwa na baadhi ya watu kushuka kimapato, kutokana na kutumia gharama kubwa katika matibabu yake.

Ugonjwa wa figo unaanza kwa hatua mbalimbali na mpaka hatua ya mwisho, mgonjwa anakuwa katika hali mbaya. Hiyo ni pale figo inashindwa kufanya kazi yake inavyopaswa, ikishughulika polepole.

Kiafya inafafanuliwa, watu wengi huwa hawaonyeshi dalili za kupona ugonjwa huo, hadi pale figo zimeharibika sana, huku kibaiolijia, figo ina kazi nyingi, ikiwamo kutoa uchafu na maji mwilini, kuzuia shinikizo la damu, kusawazisha kemikali za mwili na kuzalisha chembe za damu nyekundu.

Serikali imekuwa ikielimisha jamii namna ya kujilinda na magonjwa ya figo, kunakuwa Siku ya Figo kimataifa, inayokuwa kila mwezi Machi. Hata hivyo, inaonekana baadhi ya jamii hazina uelewa wake sahihi. Inafafanuliwa na takwimu za kiserikali kwamba, kuna Watanzania zaidi ya 800, wanahitaji huduma za kupandikizwa figo.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu, akiongea katika jengo la wagonjwa wanaosafisha figo, katika Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam, anasema tafiti zimebainisha takribani Watanzania kati ya 5,800 mpaka 8,500, wanahitaji kusafisha damu (dialysis) au huduma za kupandikizwa figo.

Akizungumzia katika maadhimisho ya Siku ya Figo Duniani anasema kuwa, hadi kufikia Januari 31 mwaka huu, kuna wagonjwa 3,250 wamepata huduma ya kusafishwa damu na wagonjwa 335 wamepandikizwa figo.

"Kati ya wagonjwa walioopandikizwa figo, wagonjwa 103 wamepandikizwa nchini, Hospitali ya Taifa ya Muhimbili imepandikiza wagonjwa 70 na Hospitali ya Benjamin Mkapa Dodoma imepandikiza wagonjwa 33,"anasema Ummy.

Anaongeza kuwa serikali imejipanga kuweka jitihada za kudhibiti na kuzuia ugonjwa wa figo na magonjwa yasiyoambukiza kwa ujumla, kwa kuimarisha afya za kinga kwa jamii.

"Naomba nikumbushe umuhimu wa kubadili mtindo wa maisha kwa kufanya mazoezi, kuepuka matumizi ya tumbaku na bidhaa zake, kupunguza matumizi ya vilevi na kuzingatia ulaji wa mlo kamili, wenye mbogamboga na matunda ya kutosha, ili kuimarisha kinga ya mwili dhidi ya magonjwa,"anasema.

Waziri Ummy anahimiza kupunguza matumizi ya chumvi, sukari na vyakula vyenye mafuta mengi na kuzingatia unywaji wa maji ya kutosha walau lita 2.5 kwa kila siku, huku kukiwapo uzingatiaji matumizi ya dawa ambazo hazijatolewa maelekezo ya kitaalamu na daktari.

Anaongeza kuwa, takwimu za Shirika la Afya Duniani (WHO) zinabainisha asilimia 10 ya watu wote duniani wanaishi na ugonjwa sugu wa figo na zaidi ni kwa wenye umri zaidi ya miaka 75, wastani wa nusu yao wana tatizo hilo.

Kuhusu utekelezaji Sera ya Afya ya Mwaka 2007 na tatizo figo, Waziri Ummy anasema serikali imeanzisha huduma za uchujaji damu kwenye hospitali za mikoa minane, kwa kuzipatia mashine 49 maalum za kazi hiyo, pia kukarabati majengo kwa gharama ya Sh. bilioni 2.8.

Anakumbusha kuwa, Tanzania huungana na mataifa mengine duniani kuadhimisha Siku ya Figo Duniani kila Alhamisi ya Wiki ya Pili ya mwezi Machi, Jumuiya ya Kimataifa ya Nefrolojia (ISN), kwa kushirikiana na Shirikisho la Kimataifa la Vyama vya Figo Duniani (IFKF), iliyoanzisha maadhimisho hayo yaliyofanyika kwa mara ya kwanza mwaka 2006.

Kaulimbiu ya mwaka huu ni 'Afya ya Figo kwa Wote- Kujitayarisha kwa yale yasiyotarajiwa kusaidia walio hatarini," ikilenga kuongeza ufahamu na elimu ya afya ya figo na kuhamasisha wananchi kujitokeza kupima afya zao.

AFYA

MIAKA MIWILI YA RAIS SAMIA

# Milima, mabonde kufikia ushindi wa vita usafirishaji haramu binadamu

## •Marekani yaipa nchi daraja; wadau waeleza magumu

**Na Zanura Mollel, LONGIDO.**

JULAI 19 mwaka jana, Waziri wa Mambo ya Nje wa Marekani, Antony Blinken, alizindua Ripoti ya Mwaka 2022 ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu kwa Tanzania, ikionekana kukidhi vigezo vya kupandishwa hadi Daraja la Pili (Tier 2).

Ni zama ambazo Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, anatimza mwaka mmoja na miezi minne kazini, akiendesha mageuzi na mikakati yake kuiendeleza nchi.

Ripoti ya Mwaka ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu, ni waraka wa jitihada za serikali kutetea hali ya binadamu, utawala wa sheria na usalama wa taifa.

Hapo inamaanisha, bado serikali nchini haijakidhi vigezo vyote vya kutokomeza usafirishaji haramu wa binadamu, lakini imefanya jitihada kubwa kudhibiti.

"Marekani imepokea kwa furaha hatua kubwa iliyopigwa na serikali ya Tanzania katika kukabiliana na usafirishaji haramu wa binadamu, ikilinganishwa na hali ilivyokuwa katika vipindi vilivyotolewa taarifa hapo awali," anatamka Balozi wa Marekani nchini, Donald Wright.

Anaendelea: "Ubalozi wa Marekani Dar es Salaam unaipongeza serikali ya Tanzania, Sekretarieti ya Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu."

Pia, anaelekeza pongezi kwa vyombo vya usimamizi wa sheria, Idara ya Ustawi wa Jamii, taasisi katika sekta ya sheria, mashirika yasiyo ya kiserikali na wabia wengine kwa mafanikio hayo, kukabili usafirishaji haramu wa binadamu.



Wahamiaji haramu waliokuwa wakisifarishwa kiharamu, chini ya ulinzi. **PICHA ZOTE: MTANDAO.**

Ripoti ya mwaka jana, imetaja hatua zilizopigwa na serikali nchini, inayojumuisha kufanyika uchunguzi wa kesi za usafirishaji haramu wa binadamu, kuwabaini waathiriwa wengi wa biashara hiyo na uratibu mzuri kitaifa na kimataifa, kuimarisha mafunzo kwa maofisa serikalini.

Hapo kunatajwa serikali ilipitisha Mpango Kazi wa Kitaifa wa Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu wa 2021 hadi 2024 na kufanywa marekebisho makubwa katika Sheria ya Kuzuia Usafirishaji Haramu wa Binadamu Mwaka 2008.

Ni jitihada zinazotajwa kufanywa kwa ushirikiano na asasi za kiraia, wanasheria wasio na mipaka na Ofisi ya Umoja wa Mataifa ya Kupambana na Dawa za Kulevya na Uhalifu.

Hapo kunaelezwa, ni kati ya serikali na asasi za kiraia katika utekelezaji shughuli za kujenga uelewa, kwa lengo la kuzuia usafirishaji haramu na kuwasaidia waathiriwa wa biashara hiyo.

"Tunaihimiza serikali ya Tanzania kupanua zaidi kazi nzuri iliyofanyika katika kipindi cha mwaka uliopita," anashauri Balozi Wright.

SURA YA MAPAMBANO

Ni wiki iliyopita, kinamama nchini wamesherehekea siku yao, huku bado wapo baadhi yao ambao wameshuhudia au wanashuhudia madhila ya aina fulani.

Hilo ni zao la ama kujua au kutokujua, kwamba sehemu ya magumu hayo huchangiwa na ndugu, pia watu waliokosa uadilifu.

Dunia ikisherehekea Siku ya Wanawake Duniani, nchini Tanzania bado wengi wanakumbwa na madhila ya usafirishaji haramu binadamu kuvuka mipaka, vilevile ndani yake ikibeba jina la 'Utumwa Mambo Leo.'

Akizungumza na Nipashe, Ofisa Mwandamizi wa Sekretarieti ya Kuzuia na Kupambana na Usafirishaji Haramu wa Binadamu katika Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi(ATS), Alexander Lupilya, anakitatafsiri 'ni kitendo cha kumsafirisha mtu, kumtumikisha kikazi pasipo malipo.'

Anaorodhesha mikoa iliyoathirika zaidi nchini ni Simiyu,Mwanza, Shinyanga, Geita, Dodoma, Singida na Dar es Salaam, hasa nyanja ya usafirishaji haramu wa binadamu nchini.



Kwa mujibu wa ofisa huyo, wanawake wengi wanasafirishwa kwa ajili ya kutumikishwa kikazi, pia ngono. Ni katika kundi la watu 150 waliookolewa kwenye matukio ya utumikishwaji, asilimia 72 na asilimia 28 iliyobaki ni watu wazima, hasa wanaopelekwa nchi za uarabuni kufanya kazi za ndani.

Inaelezwa, wapo wanawake huwekwa katika kumbi za starehe maarufu Kasino au madanguro, kutumikishwa kingono na kuna wakati, hukutana na magumu wanapokataa kuendana na ajira hiyo.

Pia anataja, saluni za kiume zinaonekana kuwa kificho cha wanawake baada ya kunyolewa wateja wa kiume. Wao huwafanyia usafi wateja na kisha kuwauliza kama wanahitaji huduma ya kingono.

Inatajwa, kuwapo baa, wanawake hawalipwi, bali wana namna ya kupata chao, ikioanishwa na ngono. Ndio kunatajawa kujitokeza kwenye migawaha na nyumba za kufanya masaji, kuna wanawake wasioajiriwa.

**HATUA ZA KISERIKALI**

Ofisa Lupilya anasema, kati ya Julai mwaka jana na mwezi uliopita, kuna kesi 13 za usafirishaji haramu wa binadamu zimepelekwa mahakamani katika mikoa mbalimbali nchini, zikiwa katika hatua mbalimbali.

Anaeleza hadi sasa, wameshawaokoa jumla ya wahanga 150 wa usafirishwaji haramu wa binadamu, waliokuwa wakitumikishwa kinguvu.

Lupilya anaainisha mchanganuo wake; kwamba 118 ni wanawake na 42 wanaume, kati yao 98 ni watoto wenye umri chini ya miaka 18, hivyo anasema ni wazi kinamama ni waathirika wakubwa wa usafirishaji huo.

Kwa mujibu wa ofisa huyo, sehemu kubwa ya matatizo wanayokumbana nayo wahanga, ni kufanyishwa kazi bila malipo, vipigo, kunyimwa chakula, kukosa haki ya matibabu wanapoumwa, kufanyishwa kazi wakiwa wagonjwa na kufungiwa ndani wasikutane na wengine.

Vilevile anataja madhila ya kulishwa makombo na hawana muda wa kupumzika wanapofanyishwa kazi za ziada, wanalala katika mazingira magumu, mfano jikoni na stoo.

Hapo Lupilya anafafanua kwamba, Sheria ya Usafirishaji Haramu wa Binadamu ya Mwaka 2008, ilikuwa ikitoa adahabu au kulipa faini, hivyo wasafirishaji wengi waliokuwa wakikamatwa walichagua kulipa faini, hata wakaachiwa huru.

Anasema, baada ya kuonekana tatizo linazidi kuongezeka, mwaka 2022 kikao cha Bunge kilifanya mabadiliko ya sheria hiyo, ikiongeza adhabu kuanzia kifungo cha miaka mitano na zaidi hadi maisha, huku faini yake ikiwa kati ya Sh. milioni tano hadi Sh.milioni 350.

Pia, ofisa huyo anaeleza kwamba imebainika kufanyika biashara hiyo, ina ukaribu wa umasikini na hali ngumu ya maisha, hivyo anatoa rai

Inaendelea Uk. 13

MAZINGIRA

## WAKATI KIMBUNGA KINATIKISA MSUMBIJI...

# Wataalamu watoa elimu madhara tabianchi; maradhi, utapiamlo...

**Na Beatrice Philemon**

INAPOZUNGUMZIWA dhana mabadiliko ya tabianchi, si watu wote wanaoifahamu vyema. Kwa miaka ya karibuni, imebainika mabadiliko ya tabianchi ni miongoni mwa majanga duniani, yanayoashiria uwezekano wa madhara makubwa kwa afya ya binadamu na ustawi wa jamii.

Hapo kunatajwa kugusa mifumo ya kijamii, kiuchumi, mazingira na maliasili, kama vile hewa safi, majisafi ya kunywa, usalama wa chakula na malazi.

Mfano ni hivi sasa inajionyesha hali ya kusambaa Kimbunga Fredy nchini Msumbiji na Malawi, ikiendelea kusambaza madhara hayo kwa wananchi kwa hali na mali zao.

Shirika la Afya Duniani (WHO) linataja kati ya mwaka 2030 na 2050, kuna mabadiliko ya tabianchi yanayosababisha takribani vifo 250,000 kila mwaka, kutokana na utapiamlo, malaria, kuhara na changamoto za joto kali.

Hivyo WHO inataja gharama za uharibifu wa moja kwa moja kwa afya, yaani pasipo kujumuisha gharama za sekta zinazohusiana na afya kama vile kilimo, maji na mazingira, kukikadiriwa thamani kuanzia Dola za Marekani bilioni mbili hadi nne kwa mwaka, ifikapo mwaka 2030.

Aidha, maeneo yenye miundombinu dhaifu ya afya hasa katika nchi zinazoendelea, yatakuwa na uwezo mdogo kuhimili mabadiliko ya tabianchi, ikiwa hakutakuwapo msaada wa kujiandaa na kukabiliana na changamoto hizo kwa wakati.

Kuhusu jitihada na mikakati inayotakiwa kufanyika, kuifanya sekta na mfumo wa afya nchini kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi, Mratibu wa Mradi kutoka Jukwaa la Mabadiliko ya Tabianchi (FORUMCC), Msololo Onditi, anasema Tanzania kama yalivyo mataifa mengine duniani, imeshuhudia athari za mabadiliko ya tabianchi kwa afya ya binadamu na jamii kwa ujumla. Anasema, dalili zinaonyesha kuwa madhara yanaweza kuongezeka siku zijazo, akitumia kauli:" Uhusiano uliopo kati ya usalama wa raia, afya ya jamii na mipango kazi ya pamoja, vinaonyesha kuna haja ya kukabiliana na madhara yanayoibuka kiafya, yakisababishwa au kuchangiwa na mabadiliko ya tabianchi, hususani upotevu na uharibifu."




Eneo lililoathiriwa na kimbunga, nchini Msumbiji. **PICHA: MTANDAO.**

Onditi anaendelea: "Mabadiliko ya tabianchi huathiri mfumo wa uzalishaji chakula, hewa tunayotumia kupumua, maji tunayokunywa na mazingira, kwa maliasili hupatikana na kutupatia mahitaji muhimu."

Kwa Watanzania wengi, anataja mabadiliko ya tabianchi huathiri ustawi na afya zao, ama kubadilika au kuongezeka ukali na kujirudia kwa madhara ya kiafya ambayo tayari jamii imekuwa ikikumbana nayo.

Pia, anasema huja na madhara ya kiafya yasiyotarajiwa kwa watu, kwa kiwango kisochowahi kutokea huko nyuma

### NINI KIFANYIKE?

Mtaalamu Onditi anaendelea: "Tukiwa wadau muhimu katika jitihada za kuhimili na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi nchini, tunapendekeza wadau kama vile vyuo vikuu na taasisi nyingine za utafiti kufanya utafiti kuhusu athari za kiafya zitokanazo na matukio yanayosababishwa na mabadiliko ya tabianchi."

Hapa ana ushauri kwamba, ni vyema kukafanyika utafiti kwa sababu kunapotokea ukame, wajawazito huathirika zaidi, hata kupata watoto wenye mapungufu kiafya, hata wanaokosa lishe kwa ukosefu wa vyakula.

Ni utafiti unaoelezwa utasaidia kujua ukubwa wa tatizo, maeneo, sekta au makundi ya watu katika jamii yaliyoathiriwa zaidi, au waliyopo hatarini kuathiriwa na mabadiliko tabianchi.

Eneo lingine analitaja ni aina ya jitihada zinazotakiwa kuchukuliwa kukabili athari hizo na kutoa mwanga kwa watunga sera, wafanya maamuzi, wabia wa maendeleo na wadau wengine, kufahamu maeneo yanayohitaji ushirikiano zaidi, sambamba na asasi za kiraia.

Tunaomba kulindwa, kuhifadhi na kurejesha mifumo ikolojia iliyoathirika au kuharibiwa ili kuimarisha hifadhi za kaboni na kupunguza hatari za mafuriko, joto kali na dhoruba ikiwemo kuunda na kutekeleza mfumo wa tahadhari ya mapema inayozingatia athari na hatari za mabadiliko ya tabianchi," anasema.

### ATHARI ZA MAFURIKO

Ofisa Mradi wa Jukwaa la Mabadiliko ya Tabianchi, Gladness Lauwo, anashauri ni muhimu kuchukua hatua za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kwa sababu mafuriko yanapotokea, husababisha kusambaa maji machafu na majitaka, maji ya kunywa kilimo, kusambaziwa kemikali, viambato vya dawa na vimelea vya magonjwa.

Lauwo anafafanua:"Mafuriko huzorotesha jitihada na hali ya usafi na kuharibu vituo vya afya. Makazi, miundo mbinu ya uhifadhi na usambazaji wa maji, mvua kubwa na mafuriko yanapopungua hutengeneza mazingira wezeshi ya kuzaliana vimelea vya magonjwa katika maeneo ambayo maji yanatuama kwa muda mrefu."

Pia, anataja afya ya uzazi na watoto kama vile kuzaliwa kabla ya wakati, vifo vya mama na mtoto na kuharibika kwa utendaji wa kijamii.

Ofisa huyo anaeleza, iwe mafuriko, ukame au kiangazi cha muda mrefu, daima huongeza uwezekano wa mtoto kupata utapiamlo na matokeo yake ya muda mrefu ni kudumaa, inayoleta athari kubwa kiafya kuanzia akili na ukuaji kimwili watoto.

Pia anataja kukithiri athari hizo kunaweza kuongezea jamii mikasa ya mfadhaiko, wasiwasi, msongo wa mawazo, matatizo ya kitabia na kiakili.

Inaelezwa, mabadiliko ya tabianchi yanaathiri makundi ya kijamii kwa viwango tofauti, kulingana na uwezo wao kuhimili hali ya kiuchumi, jamii, ufahamu na maarifa na tofauti za kijiografia.

### TANZANIA IKOJE?

Lauwo anaelezea: "Tukiangalia uwezekano wa kuathiriwa kuna watu au makundi ya watu katika jamii ambao wanaathiriwa zaidi na mabadiliko ya tabia nchi kuliko watu wengine kulingana na hali za kiafya na umri.

"Kwa mantiki hii makundi ya watu wenye magonjwa sugu na wenye kinga dhaifu ya mwili, watoto, wazee na wanawake wajawazito ni miongoni mwa makundi katika jamii ambayo yapo hatarini zaidi kuathiriwa kiafya na mabadiliko ya tabianchi."

# MILIMA, MABONDE KUFIKIA USHINDI WA VITA USAFIRISHAJI HARAMU BINADAMU

Inatoka Uk. 1

umma, kuchangamkia mbadala wa kimaisha unaojitokeza, ikiwamo serikalini .

### SHIRIKA LA WAHAMIAJI

Shirika la Wahamaji Duniani (IOM), linaeleza tafiti zilizofanywa na UNODC zimeonyesha kushuka usafirishaji haramu wa binadamu baada ya kuripotiwa mlipuko wa COVID-19

Inasema ni kipindi jamii nyingi zilikuwa karantini na wanawake wakaonekana kusafirishwa nje ya nchi kutumikishwa kingono, kwa mtindo wanapofika, hati zao za safari huzuiliwa na wenyeji wao.

"Ukishakua huna hati ya safari katika nchi ya watu unaanza kuingia matatizoni ,wengi wanaosafirishwa hurubuniwa kwa kuelezwa kupata maisha mazuri" linafafanua shirika hilo.

### KWANINI BIASHARA HARAMU?

Sababu kubwa inatajwa ni kukua soko la ngono duniani, pia hitaji la wafanyakazi wa bei rahisi katika viwanda na mashamba makubwa duniani, hali kadhalika kuwapo ushindani kati ya masikini na tajiri katika kukidhi matakwa yao.

Ofisa Uhusiano wa makao makuu ya Jeshi la Uhamiaji Tanzania, Mrakibu Msaidizi Azizi Kirondomara, anakiri usafirishaji haramu wa binadamu ndani na nje ya nchi, upo nchini ikiwamo kwa mabinti wanaosafirishwa kufanya kazi za ndani mijini, bila kulipwa stahiki, au kutolipwa kabisa na wananyanyaswa.

" Huchukuliwa kutoka mikoa ya Iringa asilimia 15; Kilimanjaro asilimia tisa na Morogoro asilimia tisa. Walichukuliwa kwenda kunyonywa katika mikoa ya Dar es Salaam, Arusha na visiwani Zanzibar.

"Hata hivyo, aina kubwa ya unyonyaji ilikuwa ni utumikishwaji kazi za ndani asilimia 55 na...(biashara ngono ) asilimia saba," anaeleza.

MAZINGIRA

## KUKITHIRI UVUVI WA MABOMU...

# Wavuvi Pwani watoa siri nyuma ya pazia hujuma zao baharini

**Na Jenifer Gilla**

MAJIRA ya saa mbili na robo usiku, Simbaeli Mudy (si jina lake kamili) mkazi wa Pemba Mnazi, Manispaa ya Kigamboni, Dar es Salaam, anasogea pembezoni mwa ukuta wa nyumba yake kuchungulia upande wa kulia kuangalia kama kuna mtu anayekuja, akijihakikishia usalama, kisha anaendelea na achokifanya.

Simbaeli anaingia stoo ya nyumba yake, anatoa chupa yenye mafuta ya petroli ujazo lita tano, yaliyochanganywa na unga kidogo wa mbolea ya urea, utambi na kibiriti, akiwa na wenzake tisa, wanaelekea ufukweni kupanda boti kwa safari ya uvuvi.

Alichokibeba Simbaeli, ni bomu ambalo yeye na wavuvi wenzake wamelitengeneza, ili kulitumia katika uvuvi, lengo ni kupata samaki wengi, jambo ambalo ni kinyume na sheria ya nchi.

Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2003, inapiga marufuku uvuvi wa mabomu, ambayo adhabu zake ni faini isiyopungua Sh.200, 000 na isiyozidi Sh. milioni 15 au kwenda jela kati ya miaka miwili hadi 10.

Nipashe inabaini uvuvi haramu katika mwalo wa Buyuni umekithiri na hufanyika katikati ya bahari majira ya usiku wa kuanzia saa saba hadi tisa, umma ukiwa usingizini.

Mvuvi Alphonce Joseph, anasema baada ya kulipuliwa mabomu katika miamba, wanapata samaki wengi, hata kuna wakati maboti hayatoshi kubeba samaki wote waliowapata, wanawaacha wengine wakielea majini.

"Sasa inategemea na wingi wa samaki unaotaka kuupata, kama unataka samaki wengi unatumia dumu la maji la lita tano, kama ni kidogo tunatumia chupa za lita mbili au lita moja na ule unga wa baruti ndio unasaidia kuleta mlipuko mkubwa," anasema.

Mtaalamu wa viumbe bahari, Jerry Mang'ena, anasema watu wengi wanajikuta wanakula samaki aliyevuliwa kwa kutomjua. Anafafanua namna ya kumtambua, anapobonyezea, eneo lililobonyezwa huwa halirudi haraka.

Pia, macho yake yanakuwa yamevilia damu, sehemu ya haja inakuwa wazi, kwa sababu mishipa iko wazi choo chake kinatoka chenyewe.



Mvuvi Jumanne Shija, akionyesha ulemavu uliotokana na shughuli za uvuvi haramu . **PICHA: JENIFER GILLA.**

### HOJA ZA KITAALAMU

Mtafiti wa viumbe bahari kutoka Chuo Kikuu Cha Dar es Salaam. Prof. Philip Bwathondi, anasema uzoefu wa muda mrefu, unambainishia uvuvi wa mabomu ndio unaoongoza nchini, ukifuatiwa na nyavu za plastiki, sababu kuu ni umasikini na kukosa elimu ya madhara yake.

"Kutokana na shughuli zao wavuvi, hawatakiwi kuwa na maisha magumu, lakini takribani asilimia 85 ya wavuvi wana hali ngumu. Bidhaa wanazovuna, wanaziuza kwa bei nafuu sana, huku madalali wakitajirika. Hiyo nayo inawasukuma kuingia kwenye biashara hiyo, ili kupata faida ya haraka," anasema Prof. Bwathondi.

Mvuvi Deus James, anasema wanakopata vifaa vya kutengeneza mabomu ya ama petroli au mafuta ya taa, huuziwa na wauzaji mafuta, huku utambi na unga unaotumika kulipua, wananunua kwa wachimba madini wanaopasulia mawe makubwa.

Mchimbaji madini kutoka Shinyanga, Remsi Chonzi, anakiri kuwapo biashara hiyo, kati ya wachimba madini na wavuvi, ingawa ana hoja, kuhusu unga wa baruti.

"Unga wanaouziwa wavuvi ni ule unaoletwa na watu wa mataifa ya Ulaya wanaokuja migodini kununua madini. Wenyewe unafanana na mbolea ya 'urea' huwa tunawauzia kwa kupima kipimo kinaanzia Sh. 30, 000 hadi Sh. 40,000 pamoja na utambi wake wa kulipulia Sh. 10,000," anafafanua.

Mang'ena, ambaye pia ni Mkurugenzi Mtendaji wa shirika la Aquafarm, anasema uvuvi wa mabomu unachangia uhaba wa samaki, kwa sababu wanakimbilia kwenye kina kirefu cha maji.

Anautaja ni aina ya uvuvi unaoathiri sana mazalia ya samaki, yakiwamo matumbawe na mapango, ambayo samaki hupendelea kutaga na kuhifadhi mayai yao, kwa utulivu uliopo.

### MIKASA NA MADHARA

Jumanne Shija (35), anasimulia mkasa wa uliompatia ulemavu mwaka 2015, baada ya kukatika kiganja cha mkono wake wa kulia, huku wenzake wanne wakifariki, alipokuwa anavua samaki akitumia bomu, hata akaacha kazi hiyo.

"Mabomu yanakuwa na utambi mfupi, kwa hiyo unapoliwasha tu unatakiwa ulitupe hapo hapo. Sasa mwenzangu alichelewa kulirusha, kwa hiyo alipoliachia likatuvuta na kututupa kwenye maji, mimi hapa nimekatika mkono na mwili wangu wote una makovu," anasimulia.

Mwenyekiti wa BMU, Pemba Mnazi, Rajabu Mkalapema, anasema kila baada ya miezi mitatu wanapokea taarifa za kifo wastani wavuvi wawili kutokana na uvuvi haramu, taarifa inayofika kutoka kwa ndugu, wahusika wakihofu kujulikana.

Magdalena Chalila, mvuvi wa Mwaloni Pemba Mnazi, anasema uvuvi haramu umewaathiri wanawake wavuvi, kwa sababu samaki wote wamekimbilia kwenye kina kirefu cha maji.

"Wanawake wengi wanavua kwenye kina kifupi cha maji, kwa kuwa hawana utaalamu wa kuogelea kwenye kina kirefu..." anasimulia na kuendelea: "...kwa sababu jua limekuwa kali na nyumba zao zimebomolewa na mabomu."

Bingwa kutoka Taasisi ya Saratani Ocean Road, Dk. Emmanuel Lugina, anaainisha mlaji samaki aliyepigwa na bomu, yupo hatarini kupatwa na saratani.

"Sasa ukiangalia mabomu ya mlipuko yanayotumika kuvua samaki, utagundua dhahiri yametengenezwa kwa kemikali mbalimbali ambazo zimehusishwa na saratani (organic amines, hydrocarbons na inorganic chemicals).

"Binadamu pia anaweza kupata madhara kwa kunywa maji au kula chakula kilichokuwa na vimelea vya kemikali zilizoko kwenye mabomu hayo," anafafanua Dk.Lugina

Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa, (FAO) linatahadharisha uvuvi haramu usioripotiwa na usiodhibitiwa, husababisha kupotea tani milioni 11 hadi 26 za samaki kila mwaka.

### VITA ILIVYO

Mwenyekiti wa Kambi ya Wavuvi Muruani Pemba Mnazi, Kigamboni, Amadi Ali, anasema wanakabiliana na shughuli hizo kwa kuweka doria na kutoa taarifa polisi, wanapobaini matendo hayo.

"Tunapobaini kuna wavuvi wanavua kinyume na utaratibu, tunatoa taarifa kwa maofisa uvuvi wanaoshirikiana na kikosi cha polisi maji na wanaweka doria kuwakamata," anasema.

Kamanda wa Polisi Kikosi cha Wanamaji Tanzania Kamishna Msaidizi, Moshi Sokoro, anasema kuna vikwazo katika kudhibiti uvuvi haramu, ikiwamo kuvujishwa taarifa za doria, hali inayokwamisha utendaji wao, katika kukabili uvuvi haramu na vifaa vyake.

Ofisa Uvuvi Kata ya Pemba Mnazi, Rahimu Said, anakiri madhila katika fukwe anazozisimamia na wanaendelea kushirikiana na viongozi wa mazingira ya usafi wa fukwe (BMU), kukabiliana nayo kupunguza mikasa na kesi, kutoka 20 mwaka 2018 hadi kesi mbili mwaka jana.

Anataja njia wanazotumia, ni doria na utaratibu maalumu wa kumtambua mgeni anayeingia mahali hapo, kwa ajili ya shughuli za uvuvi.

Prof. Bwathondi, anashauri serikali kuweka mikakati ya kuzuia uuzwaji holela vifaa vinavyotumika kutengenezea na kudhibiti uingizwaji mabomu nchini, ikiwa ni namna inayowafikia kirahisi wavuvi haramu.

Anaushauri ni wakati mwafaka kubadilisha mfumo wa kutoa elimu, kutoka kuongea kwa mdomo, hadi njia ya sinema, ili iwavutie wengi zaidi,wakiwamo watoto.





# Bunge laiagiza DUWASA kuharakisha ujenzi miradi ya maji

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

KAMATI ya Kudumu ya Bunge ya Mitaji ya Umma (PIC) imeiagiza Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mkoa wa Dodoma (DUWASA), kuharakisha ujenzi wa miradi ya maji, ili kupunguza tatizo la maji kwenye jiji hilo.

Mwenyeliti wa kamati hiyo, Jerry Silaa, alitoa kauli hiyo wakati wajumbe walipotembelea mradi wa visima vya maji Nzuguni ambao unatarajia kuzalisha asilimia 11 ya mahitaji ya maji kwa wakazi wa Jiji hilo.

Alisema kamati inaagiza DUWASA kuhakikisha mchakato wa ujenzi wa mradi mbalimbali ya maji inakamilika kwa wakati, ili kuondoa tatizo la maji kwenye jiji hilo.

Alisema kama serikali itashindwa kutoa fedha za kukamilisha miradi kwa wakati waone namna ya kukopa ili kukamilisha miradi hiyo mikubwa ya kuhudumia jamii.

Aidha, aliagiza tathmini ifanyike haraka kwa watu wanaohamishwa kupisha upanuzi wa eneo vitakapochimbwa visima hivyo.

Alisema ucheleweshaji wa tathmini hiyo unakwamisha miradi hiyo kukamilika kwa wakati.

Hata hivyo aliwapongeza DUWASA kwa ubunifu wa miradi hiyo ya kisima vilivyochimbwa maeneo mbalimbali ya Jiji kwa lengo la kutatua tatizo la maji.

Mkurugenzi wa DUWASA, Aron Joseph, alisema hali ya upatikanaji wa maji jijini Dodoma ni nusu ya mahitaji yaliyopo, hivyo mgawo lazima utaendelea.

Joseph alisema kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Makazi ya mwaka 2022, Wilaya ya Dodoma ina watu 780,000 ambao wanahitaji lita milioni 133.8 za maji, lakini kiasi kinachozalishwa kwa sasa ni nusu ya ujazi huo.

Alisema DUWASA inafanya kila namna ili kupunguza mgawo huo, lakini itachukua muda kufikia malengo hayo kutokana na ongezeko kubwa la watu kuhamia hapo.

Kuhusu mradi wa Nzuguni, alisema una unatoa maji mengi lakini bado haujaanza kufanya kazi, lakini kuna makandarasi wanaoendelea na kazi na kwamba utakamilika baada ya miezi sita.

Alisema mradi huo utagharimu Sh. bilioni 4.8 ambapo utahudumia zaidi ya wakazi 50,000 wa eneo hilo na maeneo jirani.

Aliyataja maeneo mengine yatakayonufaika na huduma hiyo ni Ilazo na Ipagala.

# Tume ya Haki Jinai yaitwa Kondoa kuona namna ukosefu wa haki unavyofanyika

**Na Paul Mabeja,** KONDOA

TUME ya kufuatilia masuala ya haki jinai nchini, imeombwa kwenda Wilaya ya Kondoa mkoani Dodoma kuona namna baadhi ya mahakimu wa Mahakama ya Mwanzo wanavyowakosesha haki wananchi.

Inadaiwa kuwa baadhi ya mahakimu wa Mahakama hiyo wanapindisha utoaji haki kwa kutoa maamuzi ya upendeleo.

Mmoja wa wakazi wa Kijiji cha Itaswi wilayani humo, Ali Kimolo, akizungumza na waandishi wa habari juzi, alisema wanaiomba tume hiyo iliyoteuliwa na Rais Samia Suluhu Hassan ikajionee muhimili huo unavyopoka haki za wananchi.

Alisema hivi karibuni alikuwa na kesi katika mojawapo ya Mahakama wilayani hapo, lakini maamuzi yalitolewa anaamini kuwa haki ilipindishwa.

"Mwaka 2019 kuna mtu alikuja kukodi shamba langu kwa ajili ya kulima nikampatia hekari 12, lakini wakati analima alizidisha hekari mbili na nusu, nilipo libaini hilo ikabidi tukae na uongozi wa kata chini ya bibi shamba na kukubaliana kuwa kiasi ambacho amezidisha mimi nitachukua mavuno heka moja na nusu na yeye atachukua heka moja tukaandikishana."

"Lakini jambo la kushangaza wakati wa mavuno nilikwenda kuvuna yeye akanishtaki kwa madai kuwa amenikuta naiba mazao yake, akafungua kesi nikashtakiwa lakini nikashinda na Mahakama ikajiridhisha kuwa hakuna kesi,"alisema.

Aidha, alisema muda mfupi baada ya kesi hiyo kuisha alifunguliwa kesi nyingine ya madai, ambapo hukumu ilitoka kuwa natakiwa kumlipa mlalamikaji Sh. milioni tisa na akishindwa dalali wa mahakama ametangaza nyumba yake pamoja na shamba la hekari zaidi ya 40 vitapigwa mnada.

Alisema hadi sasa haelewi afanye nini kwa kuwa tayari matangazo ya mnada yamesha bandikwa kwa ajili ya nyumba na shamba lake kupigwa mnada.

"Kwakweli haki zinapindishwa sana katika mahakama zetu kutokana na watu kutumia fedha zao kutukomoa sisi wanyonge, shamba langu mwenyewe nimemkodishia mtu lakini leo hii nashtakiwa kwa wizi, lakini faini ya shilingi milioni tisa ninayotakiwa kulipa haiendani kabisa na thamani ya nyumba yangu na shamba la hekari zaidi ya 40,"alisema.

Alisema anamwomba Rais Samia kupitia tume aliyoiunda ya kufuatilia masuala ya haki jinai impatie haki ambayo inakwenda kupotea kwa maamuzi ya upendeleo yanayotolewa na baadhi ya mahakimu katika Mahakama.

Naye Miraji Mbuji, alisema wanawaomba wajumbe wa tume hiyo kufika katika kijiji hicho kujionea maamuzi ya baadhi ya mahakimu ambavyo yamewakosesha haki wanayostahili na kuwapendelea wenye fedha.

Alisema tabia ya muhimili huo kupindisha haki imekuwa janga kwa wananchi wa wilaya hiyo hali ambayo kama hatua za makusudi zitachukulia watu wataamua kujichukulia sheria mkononi.

Mapema mwaka huu Rais Samia, aliunda tume ya kufuatilia masuala ya haki jinai nchini ambayo itaongozwa na Jaji Mkuu Mstaafu, Othuman Chande, akisaidia wa Katibu Mkuu Kiongozi Mstaafu, Balozi Ombeni Sefue.



Mkurugenzi Mtendaji wa Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Dodoma (DUWASA), Mhandisi Aron Joseph (kushoto), akitoa maelezo kwa wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Uwekezaji wa Mitaji ya Umma (PIC) ilipotembelea mradi wa kuboresha huduma ya maji ulioko Nzuguni jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Dodoma yaweka mikakati ya kuwavutia watalii

**Na Ibrahim Joseph,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, amesema katika kipindi cha miaka mitano mkoa huo umejipanga kukuza utalii, ili kuwavutia wageni waweze kutembelea vivutio.

Aliyasema hayo jana kwenye mkutano wake na waandishi wa habari kuhusu mfululizo wa vipindi vya kutangaza mafanikio ya taasisi mbalimbali za umma kwa Mkoa wa Dodoma, tangu Rais Samia Suluhu Hassan aingie madarakani.

Alivitaja vivutio vya utalii vilivyoko mkoani Dodoma Hifadhi ya Swagaswaga na Mkungunero ambavyo vimekuwa ni sehemu ya kuwavutia watalii wengi.

Alisema serikali imetenga Sh. bilioni nne kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya barabara ndani ya hifadhi hizo, kuboresha sehemu za malazi na maeneo ya kupumzikia wageni.

Alivitaja aina nyingine za vivutio kuwa ni kilimo cha zabibu ambacho ni zao pekee linalostawi kwenye ukame na linastawi mara mbili kwa mwaka.

Senyamule alitaja vivutio vingine ni eneo la mahandaki ya wapigania uhuru ya askari wa nchi za Kusini mwa Afrika katika Wilaya ya Kongwa pamoja na majengo na mji wa serikali.

Aitaja vivutio vingine ni michezo na viwanja vya ndege hasa Uwanja wa Msalato wenye uwezo wa kutua ndege kubwa za kitaifa na mataifa. Kamishna Msaidizi Mwandamizi wa Uhifadhi Shirika la Hifadhi (TANAPA), Dk. Noelia Myonga, alisema mpaka sasa kuna hifadhi 22 nchini na zina ukubwa wa kilomita za mraba 104,464 sawa na asilimia 51 ya eneo la nchi.

Alibainisha kuwa TANAPA imepewa jukumu la kusimamia na kutangaza vivutio vilivyoko kwenye hifadhi hizo ili kuliingizia taifa mapato.

Hata hivyo alimpongeza Rais Samia Suluhu Hassan kwa kusaidia kuwavutia watalii wengi kutokana na filamu ya Royal Tour ambayo imeongeza idadi kubwa ya watalii nchini.

Dk. Myonga alisema mafanikio hayo ni sehemu ya TANAPA kusherehekea mafanikio yaliyopatikana miaka miwili ya uongozi wa Rais Samia.

Kadhalika, aliwataka wananchi kuwa na tabia ya kutembelea vivutio vilivyoko nchini kwa sababu gharama zake ni ndogo kulinganisha na wageni kutoka nje.



# TRIT yahamasisha wakulima kutumia kilimo cha umwagiliaji

**Na Nebart Msokwa,**
MBEYA

TAASISI ya Utafiti wa Chai nchini (TRIT) imeanza kuhamasisha wakulima wadogo wa zao hilo kuanzisha mifumo ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji.

Mkurugenzi wa TRIT, Dk. Emmanuel Simbua, aliyasema hayo wakati wa ziara ya ukaguzi wa miradi mbalimbali inayotekelezwa kupitia programu ya uboreshaji wa mnyororo wa thamani wa kahawa, chai na mazao ya bustani ijulikanayo AGRI-CONNECT.

Programu hiyo inafadhiliwa na Umoja wa Ulaya (EU) na kutekelezwa katika mikoa maeneo mbalimbali nchini ambapo kwa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini inatekelezwa katika mikoa ya Mbeya, Songwe, Katavi, Iringa na Ruvuma.

Dk. Simbua alisema kilimo cha umwagiliaji kwenye chai kinamwongezea mkulima uzalishaji kwa asilimia 40 na kwamba endapo wataongeza na matumizi ya mbolea kuna uwezekano wa tija kufikia asilimia zaidi ya 60.

Alisema wamefanya majaribio katika maeneo mbalimbali nchini yanayolima zao hilo na kwa sasa wanaendelea na uhamasishaji kwa wakulima, huku akikisisitiza kuwa wanakusudia kuchimba visima kwenye maeneo ambayo yana uhaba wa maji.

"Tunataka wakulima wadogo wafikie tija inayofikiwa na wakulima wakubwa, kwa huku Rungwe tunaendelea na mifumo miwili ya umwagiliaji ambayo ni mfumo wa matone na mfumo wa unyunyiziaji na tunataka wakulima watoke maeneo mengine waje kujifunza hapa," alisema Dk. Simbua.

Alisema walianzisha mashamba ya mfano katika baadhi ya maeneo wilayani Rungwe kwa ajili ya kufundishia wakulima na kwamba mpaka sasa wakulima wengi wameshaanza kununua vifaa na kuomba kufungiwa kwenye mashamba yao.

Mwenyekiti wa Chama cha Wakulima wa Chai Masebe (Masebe AMCOS), Sales Mwakanyamale, alisema kwenye mashamba ambayo wameyafanyia majaribio kwenye umwagiliaji wameanza kuona mabadiliko.

Alisema kwenye moja ya mashamba ambayo walifanyia majaribio kwa kutumia mfumo wa kunyunyiza walibaini kuwa uzalishaji uliongezeka kwa maelezo kuwa awali walikuwa hawana uwezo wa kufikisha kilo 300 kwa mchumo mmoja, lakini baada ya kumwagilia walifikisha kilo 500.

Alisema mbali na ongezeko hilo la mavuno pia muda wa uchumaji uliongezeka, kwamba wanavuna mwaka mzima tofauti na awali ambapo wakati wa kiangazi walikuwa wanasitisha uvunaji kutokana na majani kushindwa kuchipua.

Ofisa Kiungo wa Programu ya AGRI-CONNECT kutoka Wizara ya Kilimo, Daines Mtei, aliishukuru EU kwa kufadhili programu akisema inaleta tija kwa mkulima na taifa.

Alisema Wizara ya Kilimo itaendelea kutoa elimu kwa wakulima waliowezeshwa kupitia programu hiyo ili wawe na uwezo wa kuendeleza miradi hiyo hata baada ya programu hiyo kufikia ukomo mwakani.

Mwakilishi wa EU, Andrea Maccarelli, alisema jumuiya hiyo inaridhika na namna ambavyo programu hiyo inatekelezwa hasa kwa kuwagusa moja kwa moja wakulima wadogo.

Alisema EU itaendelea kushirikiana na Tanzania katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo hasa katika sekta ya kilimo na lishe ili kukabiliana na matatizo ambayo yanawakabili wananchi.




Naibu Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa (wa pili kushoto), akipata maelezo kutoka kwa Ofisa Masoko na Mawasiliano wa Kampuni ya GF Trucks & Equipment's Ltd, Smart Deus, alipotembelea maonyesho ya teknolojia ya madini yanayoendelea wilayani Chunya mkoani Mbeya jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Hospitali ya Kanda yatoa mafunzo magonjwa ya damu

**Na Nebart Msokwa,** CHUNYA

HOSPITALI ya Kanda ya Rufani ya Mbeya, imeanza kutoa mafunzo kwa watumishi wa afya wa hospitali za wilaya kuhusu magonjwa ya damu ili waweze kuyakabili, ikiwamo ugojwa wa kuganda kwa damu.

Juzi madaktari bingwa wa magonjwa hayo walitoa mafunzo kwa watumishi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya ambako kunadaiwa kuna ongezeko la watu wanaosumbuliwa na magonjwa ya damu.

Daktari Bingwa wa Magonjwa ya Damu kutoka Hospitali ya Kanda ya Rufani Mbeya, Dk. Mathia Ishengoma, alisema waliamua kutoa mafunzo hayo ili wagonjwa wa magonjwa hayo wanapopatikana waweze kupata huduma mapema.

Alisema baadhi ya wagonjwa ambao wamekuwa wakibainika kuwa na magonjwa hayo wamekuwa wakipelekwa katika Hospitali ya Kanda jambo ambalo linaweza kuhatarisha zaidi maisha yao. Alisema mafunzo hayo yaliwahusisha watumishi wote wa hospitali ili kupanua zaidi wigo wa utoaji wa huduma hizo kwa wananchi wa maeneo hayo.

Baadhi ya washiriki wa mafunzo hayo waliwashukuru madaktari bingwa hao kwa kuwapatia mafunzo hayo wakieleza kuwa ni miongoni mwa nyenzo muhimu ambazo watazitumia katika kuokoa maisha ya wananchi.

Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya, Dk. Ally Msonga, alisema mafunzo hayo yaliwapatia utaalamu wa kuwahudumia wananchi watakaobainika kuwa na matatizo hayo kwa weledi tofauti na ilivyokuwa awali.

Alisema magonjwa ya damu huwa hayawakumbi mara kwa mara wananchi lakini wanahitaji kujiandaa ili inapotokea wawe na uwezo wa kuyakabili kirahisi.

Ofisa Muuguzi Msaidizi wa Hospitali ya Wilaya ya Chunya, Pascalina Mwaipopo, alisema mafunzo waliyoyapata yatawasaidia kuwatambua watu wenye matatizo ya hemofilia na kuwatibu kirahisi.

# Wakurugenzi h'shauri waagizwa kusimamia mifumo ya afya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

SERIKALI mkoani Mbeya imewaagiza wakurugenzi wa halmashauri za mkoa huo kusimamia mifumo ya afya ikiwamo mfumo wa manunuzi, ili kupunguza matatizo ambayo yamekuwa yakitokea mara kwa mara.

Aidha, wametakiwa kushirikiana na wataalamu wa afya kufanya ukaguzi wa dawa mara kwa mara kwenye vituo vya kutolea huduma za afya na kuziondoa dawa ambazo zitabainika kuwa muda wake wa matumizi umekwisha.

Katibu Tawala wa Mkoa wa Mbeya, Rodrick Mpogolo, alitoa agizo hilo juzi jijini Mbeya alipofunga mafunzo maalumu ya usimamizi wa manunuzi kwenye sekta ya afya yaliyoandaliwa na Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI).

Washiriki kwenye mafunzo hayo ni wakurugenzi wa halmashauri, waganga wakuu, maofisa afya, wataalamu wa maabara, wataalamu wa TEHAMA na wafamasia wa halmashauri.

Mpogolo alisema matatizo mbalimbali yamekuwa yakiibuka kwenye vituo vya kutolea huduma za afya kutokana na usimamizi mbovu wa wakurugenzi wa halmashauri ambao ndiyo watendaji wakuu wa maeneo hayo.

Alisema serikali iliamua kuanzisha mfumo wa kuwatumia washitili ili kuziba pengo kwenye maeneo ambayo Bohari ya Dawa (MSD) inashindwa kuhudumia.

Alisema serikali inatumia fedha nyingi kwenye sekta ya afya ikiwamo ununuzi wa dawa, lakini usimamizi ukiwa mbovu, tija itakuwa ndogo.

Mwakilishi wa Mganga Mkuu Mkoa wa Mbeya, Dk. Patrick Kibopile, aliwataka washiriki wa mafunzo hayo kuhakikisha wanakuwa makini wakati wa mafunzo ili waelewe wanachofundishwa.

Alisema wamechukuliwa wachache kwenda kupata mafunzo hayo ili baada ya kukamilisha na wao wakasambaze elimu hiyo kwa wenzao ambao wamebaki kwenye vituo vya kazi.

Alisema lengo la serikali ni kuhakikisha inaimarisha mifumo ya utoaji wa huduma kwa wananchi katika sekta hiyo hasa kuimarisha upatikanaji wa dawa na vifaa tiba.



# Watumishi Maji waonywa kufanya kazi kwa mazoea

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WATENDAJI wa Wizara ya Maji, Nishati na Madini, wametakiwa kuacha kufanya kazi kwa mazoea bali wafanye kwa mujibu wa sheria na mikataba yao ya kazi.

Rai hiyo imetolewa na Mkurugenzi wa Sera na Utafiti wa wizara hiyo, Mariam Issa Juma, wakati akifungua mafunzo ya sheria na kanuni za utumishi wa umma kwa watendaji wa wizara hiyo.

Alisema katika kufikia malengo ya wizara hiyo ni lazima watendaji wawe tayari kufanya kazi kwa mujibu wa miongozo yao na kuacha kufanya kazi kwa mazoea.

Juma alisema watumishi wa umma wanajukumu kubwa la kuwatumikia wananchi katika kutoa huduma bora kwa mujibu wa kanuni za utumishi wa umma.

"Watumishi wa umma lazima mfanye kazi kwa mujibu wa mikataba yenu ya kazi kwa kuwatumikia wananchi kwa mujibu wa sheria,"alisema.

Akitoa mada katika mafunzo hayo kuhusu rushwa, Ofisa Elimu kutoka Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA), Yussuf Juma, alisema serikali inachukua jitihada mbalimbali katika kuzuwia na kupambana na vitendo vya rushwa, hivyo ni vyema watumishi wa umma na wananchi wakapewa elimu hiyo.

Alisema mapambano ya rushwa siyo jukumu la ZAECA pekee bali kila mmoja anajukumu hilo kwa nafasi aliyonayo, hivyo aliwataka watumishi hao kufanya kazi kwa kufuata sheria, kanuni na taratibu na bila ya kuendeleza vitendo vya rushwa katika utekelezaji wa majukumu yao.

Ofisa huyo aliwataka watumishi hao kuunga mkono jitihada za serikali katika kuzuwia na kupambana na rushwa katika utumishi wa umma kwa lengo la kuleta maendeleo nchini na ustawi wa jamii.

Alisema uelewa wa wananchi katika mapambano ya rushwa uelewa unaongezeka na wapo wanaotoa taarifa mbalimbali za vitendo vya rushwa na uhujumu wa uchumi.

"Lengo letu ni kufikia asilimia sifuri ya rushwa na wananchi washindwe kuvumilia kuona vitendo vya rushwa vinafanyika...mapambano ya rushwa na uhujumu wa uchumi hayahitaji nguvu za vita bali kila mmoja kuwa tayari kutoa taarifa,"alisema ofisa huyo.

Baadhi ya watendaji waliopatiwa mafunzo walisema mafunzo hayo yamewajengea uelewa mkubwa juu ya kufanya kazi zao kwa kufuata miongozo ya kazi na sheria za kazi lakini kujua wajibu na haki zao.




Waziri wa Biashara na Viwanda Zanzibar, Omar Said Shabadi (wa nne kulia), akikabidhi mfano wa hundi yenye thamani ya Sh. milioni 578 kwa wananchi wa kijiji cha Dunga, ikiwa ni malipo ya fidia baada ya eneo la ardhi yao kuchukuliwa na serikali kwa ajili ya uwekezaji wa viwanda Mkoa wa Kusini Unguja jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Profesa aeleza faida zitakazopatikana uwapo vazi la taifa

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MWENYEKITI wa Kamati ya Vazi la Taifa, Prof. Hermans Mwansoko, amesema kuwapo kwa vazi la taifa ni njia moja wapo ya kuitangaza nchi kimataifa.

Aliyasema hayo jana wakati wa mkutano wa kukusanya maoni kwa wadau juu ya kuwapo wa utambulisho wa vazi la taifa.

Profesa Mwansoko alisema kuwapo kwa vazi hilo kutaifanya Tanzania kujulikana zaidi na kuwapo kwa vazi hilo haina maana ya kuwa kila mtu lazima alivae wakati wote.

Mwenyekiti huyo alisema kamati hiyo kazi yake kubwa ni kukusanya maoni wa wadau mbalimbali juu ya kuwapo kwa jambo hilo na baadaye kamati inayachukuwa na kuyafanyia kazi kama inavyo takiwa.

"Tumeamua kuja Zanzibar kukusanya maoni ili kuona namna gani Wazanzibari wanatoa maoni yao kuhusu vazi hilo,"alisema.

Katibu Mtendaji wa Baraza la Sanaa, Sensa ya Filam, Dk. Omar Abdallah Adam, alisema kamati hiyo kufika Zanzibar na kuchukuwa maoni ya wadau ni moja ya kufanya kazi kwa pamoja.

Alisema kupatikana kwa vazi la taifa ni moja ya nafasi muhimu ya kuitangaza Tanzania kimataifa na itamwezesha Mtanzania kutembea na utambulisho wake.

Mbunifu wa mavazi, Mustafa Arsanali, alisema kuna umuhimu mkubwa wa kuwapo kwa vazi hilo kwa kuwa litaitambulisha nchi katika mataifa mingine.

Alisema kuwapo kwa vazi hilo ni nafasi moja lakini lazima kuwe na vazi ambalo lilolokuwa na ubunifu mzuri ili kuendana na matakwa ya taifa.

# Spika awapa mbinu wajasiriamali kufanikiwa kimaisha

**Na Mwandishi Wetu**

WAJASIRIAMALI wametakiwa kuingia katika mfumo wa teknolojia ya kibiashara ambao utawawezesha kufanya shughuli zao kwa mafanikio kutokana na mageuzi ya kibiashara yaliopo sasa.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi, Mgeni Hassan Juma, wakati akizungumza na wajasiriamali wanawake ikiwa ni sehemu ya maadhimisho ya Siku ya Wanawake Duniani.

Alisema wakati umefika sasa shughuli za ujasiriamali kufanyika katika mazingira ya teknolojia ya kimtandao ambayo itawawezesha kutafuta masomo bora sehemu yoyote duniani.

Aidha, aliwataka wajasiriamali kuchangamkia fursa za mikopo iliyotolewa na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa ajili ya kufanya biashara.

Alisema kwa mara ya kwanza serikali imetenga fedha kwa wajasiriamali ambao wanafuga wa nyuki, Sh. milioni 780 ambazo zitawawezesha kutekeleza malengo yao ya kibiashara.

"Wajasiriamali wanawake huu ni wakati wa kufanya shughuli zenu kimaendeleo zaidi kwa kutumia teknolojia ya kimtandao kwa ajili ya kutafuta masoko,"alisema Mgeni.

Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwezeshaji, Mariyam Abdalla Sadalla, alisema Serikali ya Zanzibar imetenga Sh. bilioni 47.3 kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kiuchumi na ujasiriamali.

Alisema katika fedha hizo zipo Sh. bilioni 28.8 ambazo zimetengwa kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kuingia katika uchumi wa buluu, ambao unawahusisha makundi mbalimbali ikiwamo wanawake.

Alisema katika uchumi wa buluu serikali inakusudia kujenga kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya bidhaa samaki aina ya dagaa.

Aidha, alisema serikali imetenga Sh.bilioni 2.5 kwa ajili ya kujenga kiwanda cha kusarifu na kuongeza thamani ya mwani eneo la Chamanangwe Mkoa wa Kaskazini Pemba.

"Hizo ni fursa za wanawake kiuchumi kwa wajasiriamali pamoja na wanawake kuingia katika uzalishaji wa mazao ya baharini ikiwamo mwani ambapo soko lake lipo kubwa lenye tija,"alisema.

Katibu Mkuu Wizara ya Uvuvi na Uchumi wa Buluu, Dk. Suleiman Aboud Jumbe, alisema tayari wizara imetengeneza boti za uvuvi 500 ambazo zitatumiwa kwa ajili ya wakulima wa mwani.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**DONNELL PATRICE MATAFU** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA COROLLA** yenye usajili namba: **T309 AGP, CHASSIS** NAMBA: **EE1115040712** na ENGINE NAMBA: **4E2418543.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **ARU/ARU/RB/97072/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ALLY RAMADHANI MNG'ONG'O,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HARRIER,** Yenye no za Usajili **T-718-DBA,** Yeyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi. TAARIFA YA POLISI: **DOD/DOD/RB/96242/2023**

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**

**SHAURI NA.94/2022**

**JOSEPHINA NDINA NOEL MBISE......................................MDAI**

**DHIDI YA**

**1; JAILOS DOYA ..................................................MDAIWA**
**2; ZIADA MBUNA ..................................................MDAIWA**
**3; JUSTIN NDABI MWAMBONEKE.........................MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA; JUSTIN NDABI MWAMBONEKE**

Fahamu kwamba JOSEPHINA NDINA NOEL MBISE amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 20/03/2023 saa 2:30 asubuhi mbele ya T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.
**Kumbuka;** Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri /muhuri wa baraza hili leo tarehe 07/03/2023.

**MAHAKAMA YA ARDHI NA NYUMBA YA WILAYA YA MBEYA**

**SHAURI NA.94/2022**

**JOSEPHINA NDINA NOEL MBISE......................................MDAI**

**DHIDI YA**

**1; JAILOS DOYA ..................................................MDAIWA**
**2; ZIADA MBUNA ..................................................MDAIWA**
**3; JUSTIN NDABI MWAMBONEKE.........................MDAIWA**

**YAH: KUITWA SHAURINI**

**KWA; JUSTIN NDABI MWAMBONEKE**

Fahamu kwamba JOSEPHINA NDINA NOEL MBISE amefungua shauri dhidi yako katika baraza hili.

Shauri limepangwa kutajwa tarehe 20/03/2023 saa 2:30 asubuhi mbele ya T.Munzerere Mwenyekiti wa Baraza.Unatakiwa kuleta utetezi wa maandishi ndani ya siku 21 tangu tarehe ya wito huu. Nyaraka zinazohusu shauri hili zinapatikana katika masijala ya Baraza la Ardhi na Nyumba Mbeya.

Unaamriwa kuhudhuria mbele ya Baraza siku hiyo bila kukosa wewe mwenyewe au mwakilishi wako anayeruhusiwa kisheria.Ofisi za Baraza zipo ndani ya eneo la sabasaba Mbeya mjini.
**Kumbuka;** Usipohudhuria siku hiyo baraza litatoa amri stahilivu ikiwa ni pamoja na kusikiliza shauri pasipo wewe kuwepo.
Amri hii imetolewa kwa mkono wangu na lakiri /muhuri wa baraza hili leo tarehe 07/03/2023.

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**LAWRENT GWAMAKA KOROSSO** anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 123 CEE.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/URA/RB/97192/2023.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**JUSTINE DAUSON MMBANDO** anatangaza kupotea kwa kadi ya Gari yenye jina **VICTOR LUCAS KWEKA** yenye namba za usajili **T 554 AUY** aina ya **BUS,** Chassis No. **FK417KZ740036.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya polisi **DOD/KON/RB/73493/2023.**

**FORM NO. 58**
**IN THE COURT OF DISTRIC T DELEGATE OF MOROGORO**
**DISTRICT AT MOROGORO**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO 23 OF 2023**

**In Matter of the Estate of the Late RUWAICHI PAULO MAMBALI**
**By 1. ASANAEL GILBERT MAMBALI**
**2. .................................**

All Persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of probate (or latter of administration) is made to the above - named petitioner.
Objection to the grand should be field on or before the **04** day of **4 / 2023.**
Dated at **Morogoro**, this **15** day of **03, 2022**

RESIDENT MAGISTRATE

## KUPOTEA KWA CHETI



**NUHU MSOLA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0515/0170** kilichotolewa na baraza la mitihani la taifa kupitia **ILULA SECONDARY SCHOOL** mwaka 2007. Kwa yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. **POLISI TAARIFA: IRI/RB/7434/2017**

***OFISI ZA MATANGAZO***

***Mikocheni Industial Area,***

***Po.Box 31042, Dar es Salaam.***

***Mobile: +255 - 745 700 710.***

***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***

***Website: www.ippmedia.com***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# Marekani, Russia zatupiana lawama kuangushwa drone

**WASHINGTON, Marekani**

MAREKANI imeishutumu Russia kwa kile ilichokiita uzembe baada ya ndege yake isiyokuwa na rubani kuanguka kwenye Bahari Nyeusi kufuatia kugongana na ndege za kijeshi za Russia.

Kabla ya kugongana, ndege za Russia aina ya jet zinasemekana zilimwaga mafuta katika njia ya droni , ambayo Marekani ilisema ilikuwa anga za kimataifa.

Droni aina ya MQ-9 Reaper iliangushwa Jumanne baada ya makabiliano yaliyodumu kwa muda wa dakika kati ya 30 na 40.

Hata hivyo, Russia ilikanusha kwamba ndege zake aina ya jet Su-27 zilizofanya mawasiliano zilihusika.

Bado haijafahamika kama mgongano huo ulikua ni jaribio la Russia kuvuruga droni ya Marekani katika kazi yake, au iwapo lilikuwa ni jaribio la kuiangusha chini kwa makusudi. Maofisa wa kijeshi wa Marekani walisema tukio hilo lilitokea saa moja na dakika tatu siku ya Jumanne.

Taarifa hiyo ya Marekani ilisema mara kadhaa kabla ya mgongano huo, ndege za kivita ziliangusha mafuta kwenye droni kizembe, bila kujali mazingira.

"Ndege yetu ya MQ-9 ilikuwa katika operesheni yake ya kawaida katika anga la kimataifa ilipopigwa na ndege ya Russia, na kusababisha kuanguka na kupotea kabisa kwa MQ-9." ilisema taarifa hiyo.

Katika jibu lake kwa Marekani, Wizara ya ulinzi ya Russia ilisema kuwa droni ilianguka baada ya kukwepa kwa ujanja na kuongeza kuwa ilikuwa inasafiri huku vifaa yake vya mawasiliano vikiwa vimezimwa.

***BBC***



Baadhi ya raia wakitafuta watu walionusurika katika dhoruba iliyosababishwa na kimbunga Freddy kilichopiga jiji la Blantyre nchini Malawi juzi. **PICHA: AFP**

# Wanajeshi Malawi wasombwa maji

**BLANTYRE, Malawi**

WANAJESHI wawili wa Malawi walitoweka baada ya boti lao la uokoaji kusombwa na maji katika eneo la Mulanje kusini mwa Malawi.

Gazeti la New York Times, lilimnukuu msemaji wa jeshi wa nchi hiyo akisema kuwa ujumbe huo ulitatizwa baada ya mto kujaa maji.

Askari hao walikuwa ni sehemu ya wafanyakazi sita waliokwenda kuokoa watu waliokwama baada ya Kimbunga cha Tropiki Freddy, kukumba eneo hilo.

Waziri wa Serikali ya Mtaa, Richard Chimwendo Banda, aliambia chombo hicho cha habari wanajeshi wengine wawili na raia mmoja walifanikiwa kuogelea na kujiokoa baada ya boti yao kupata hitilafu ilipokuwa njiani.

Banda alisema mmoja wa askari hao alietoweka alionekana kwenye mti na juhudi za kumwokoa zilifanyika.

Dhoruba ya kimbunga Freddy, iliyovunja rekodi ambayo ilitua katika taifa hilo imesababisha vifo vya watu zaidi ya 200.

Kituo cha kibiashara cha Malawi, cha mjini Blantyre, kilishuhudia maiti ya watu wakiwemo watoto.

Mamlaka imechelewesha kufunguliwa kwa shule hadi Ijumaa na kutangaza hali ya dharura katika wilaya 10 za kusini ambazo zimeathiriwa zaidi na kimbunga hicho.

Serikali ya Malawi imethibitisha zaidi ya watu 200 wamefariki dunia kutokana na kimbunga Freddy kukumba eneo la kusini mwa Afrika kwa mara ya pili ndani ya mwezi mmoja.

Imeelezwa maafa makubwa yametokea katika wilaya 10 za kusini mwa Malawi.

Wafanyakazi wa uokoaji walionekana kuzidiwa kutokana na kutumia zana duni kama majembe wakijaribu kuwatafuta watu walionusurika.

"Tuna mito inayofurika maji, tuna watu waliobebwa na maji ya bomba, tuna majengo yaliyoporomoka," alisema msemaji wa polisi Peter Kalaya.

Msemaji huyo alikumbuka jinsi alivyosaidia kumwokoa mtoto, mkazi wa Blantyre, asisombwe na maji.

"Mtoto huyo alikuwa amekwama kichwani kwenye tope, alikuwa akilia kuomba msaada, japokuwa maji yalikuwa makali sana, tulifanikiwa kuvuka na kumuokoa, ilikuwa ngumu sana lakini tuliweza kumtoa nje." alisema

Maofisa katika hospitali kuu ya rufaa mjini humo, walisema hawawezi kukabiliana na idadi kubwa ya miili ambayo walikuwa wakiipokea.

Shirika la misaada la kimatibabu la Madaktari Wasio na Mipaka lilisema kuwa zaidi ya watoto 40 walitangazwa kufariki dunia walipofika hospitalini.

Viongozi walitoa wito kwa familia za marehemu kuchukua maiti kwa ajili ya mazishi kutokana na chumba cha kuhifadhia maiti cha hospitali hiyo kukosa nafasi.

***BBC***

## Blinken kupunguza joto la vita Tigray

**ADDIS ABABA**

WAZIRI wa Mambo ya Kigeni wa Marekani Antony Blinken, amekutana na waziri mwenzake wa Ethiopia Ababa Demeke Mekonnen kwa ajili ya mazungumzo.

Mawaziri hao wanakutana wakati serikali zao zikilenga kurekebisha mahusiano kufuatia HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/ethiopia-yatoa-onyo-juu-ya-uchunguzi-wa-vita-vya-kaskazini/a-64714193" misuguano iliyotokana na vita vya wenyewe kwa wenyewe vilivyodumu miaka miwili katika jimbo la Tigray.

Waziri Blinken kisha atakutana na Waziri Mkuu Abiy Ahmed na viongozi wa vikosi vya Tigray ambavyo vilikabiliana na serikali ya shirikisho katika HYPERLINK "https://www.dw.com/sw/waasi-wa-tigray-waanza-kuzisalimisha-silaha-zao-nzito/a-64350197" vita vya jimbo hilo.

Serikali na vikosi vya Tigray wametiliana saini ya kumaliza vita hivyo, huku wanajeshi wa serikali ya shirikisho wakianza kulinda usalama jimboni humo.

Baada ya kumaliza ziara nchini humo kiongozi huyo ataelekea katika taifa la Afrika Magharibi la Niger, huko atazungumzia njia ya kupambana na ongezeko la uasi wa itikadi kali.

***DW.***

## Polisi Ujerumani yasaka mtandao haramu

**BERLIN, Ujerumani**

POLISI wa Ujerumani wamefanya msako mkali kuwasaka wanachama wa kundi la watu wanaoshukiwa kuwa wasafirishaji haramu wa binadamu.

Karibu maofisa 400 wa polisi, miongoni mwao wa shirikisho na wa vitengo maalum, walipekua zaidi ya nyumba 20 na ofisi, katika mji mkuu Berlin na jimbo la mashariki la Saxony-Anhalt.

Shirika la habari la Ujerumani (DPA) limesema wanaume watano walikamatwa, wanne kati yao mjini Berlin na mmoja katika mji wa Halle. Washukiwa wengine 12 wakiwekwa chini ya uchunguzi.

Kundi hilo linadaiwa kuwaingiza nchini Ujerumani karibu watu 90, wengi wao kutoka Uturuki na Iraq.

Polisi ilisema wahamijai hao kila mmoja alilipa maelfu ya Euro, na idadi kubwa ya washukiwa hao wana uraia wa Uturuki au Ujerumani.

***DW.***

HABARI MICHEZO

# DILUNGA AREJEA KIKOSINI, ASUBIRIWA ROBERTINHO

**Na Saada Akida**

HATIMA ya aliyekuwa kiungo mshambuliaji wa Simba, Hassan Dilunga, kuendelea kukitumikia kikosi hicho katika msimu ujao iko mikononi mwa benchi linaloongozwa na Kocha Mkuu, Roberto Oliviera 'Robertinho' imeelezwa.

Dilunga amerejea rasmi katika mazoezi ya timu hiyo yaliyofanyika kwenye Uwanja wa Mo Simba Arena juzi baada ya kukaa nje kwa zaidi ya mwaka mmoja akiuguza jeraha.

Akizungumza na gazeti hili jana, Meneja wa Idara ya Habari na Mawasiliano wa Simba, Ahmed Ally, alisema Dilunga yuko ndani ya timu hiyo kwa ajili ya uangalizi zaidi chini ya daktari, Edwin Kagabo pamoja na Robertinho.

Ahmed alisema kurejea kwa nyota huyo ni kumwangalia kwa ukaribu huku benchi la ufundi kupata nafasi ya kumwona ili kujiridhisha kabla ya kufanya uamuzi wa kumpa mkataba mpya wa kuitumikia Simba katika msimu ujao.

"Dilunga alipata jeraha akiwa ndani ya kikosi cha Simba na muda wote alikuwa akihudumiwa na klabu yake, licha ya kufanya mazoezi katika vituo mbalimbali lakini sasa amerejea na ndani ya klabu na kuangaliwa kwa umakini zaidi," alisema na aliongeza;

Ataendelea kufanya mazoezi chini ya uangalizi, mustakbali wa nyota huyo kupewa mkataba na kucheza msimu ujao utaamuliwa na benchi la ufundi na daktari watavyojiridhisha na kiwango chake watakachokiona katika kipindi chote anachokuwa hapa kikosini," alisema Ahmed.

Aliongeza Simba haitakuwa wajinga kumwacha nyota huyo ambaye ni dhahabu katika soka la hapa nchini.

Daktari wa Simba, Kagabo aliliambia gazeti hili alikuwa anamfanyia uchunguzi nyota huyi ili kufahamu kama ameimarika.

Dilunga alisema baada ya kupona majeraha amerejea mazoezini na kuendelea kufanya mazoezi chini ya uangalia wa daktari Simba.

Alisema mkataba na Simba umemalizika na kipindi chote alichokuwa majeruhi alisaidiwa na klabu hiyo.

"Laiti kama Simba wasingenihudumia kipindi chote ambacho nilikuwa na majeraha basi hii leo (jana), nisingerudi tena, nitakuwa sehemu ya wachezaji wa timu hii hadi msimu ujao nitakapoongeza mkataba.

Natamani kuwa sehemu ya kikosi watakaosaidia Simba katika mapambano lakini bado sijakuwa fiti na mambo ya kimkataba, ninaimani na wachezaji wenzangu katika hiki kipindi cha kuipeleka timu kucheza hatua ya robo fainali," alisema Dilunga.

Mbali na kucheza mechi nyingi, lakini wanachama na mashabiki wa Simba wanamkumbuka zaidi kwa bao lake alilolifunga Desemba 2, 2021, nchini Zambia dhidi ya Red Arrows ambalo liliihakikishia timu hiyo kutinga hatua ya makundi ya michuano ya Kombe la Shirikisho Afrika.

Katika mechi hiyo Simba ilifungwa mabao 2-1, lakini ikinufaika na ushindi wa mabao 3-0 ilioupata nchini Novemba 28, mwaka huo.




Shabiki wa soka, Nobert Ngangala wa Mbezi, Dar es Salaam akiwa amekamilisha mchakato wa usaili na kupatiwa tiketi ya kushuhudia mechi ya Simba na Yanga itakayochezwa Aprili 16, mwaka huu baada ya kushinda Promosheni ya Betika Mtoko Kibingwa. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Hat-trick sita zafungwa Bara

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI zikiwa zimebaki raundi tano ili kumalizika kwa Ligi Kuu Tanzania Bara, tayari 'hat-trick' sita zimepatikana kupitia kwa wachezaji watano.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, Simba inaongoza kwa kuwa na 'hat-trick' nyingi zaidi ikiwa nazo nne, huku wachezaji wake wakiongoza pia.

Timu hiyo ina wachezaji watatu waliofunga hat-trick hizo ambao ni nahodha, John Bocco, Saido Ntibazonkiza na Jean Baleke.

Bocco ndiye mchezaji aliyefunga hat-trick mbili msimu huu, huku Ntibazonkiza na Baleke wakifunga moja.

Jumamosi iliyopita, straika raia wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo, Baleke alifunga 'hat-trick' yake ya kwanza tangu atue nchini wakati Simba ikicheza dhidi ya Mtibwa Sugar na kupata ushindi wa mabao 3-0.

Straika wa Yanga, Fiston Mayele yupo kwenye orodha ya wachezaji waliofunga mabao matatu kwenye mechi moja, akifanya hivyo Desemba 20, mwaka jana kwenye mechi dhidi ya Singida Big Stars iliyomalizika kwa mabingwa hao watetezi kupata ushindi wa mabao 4-1.

Januari 23 mwaka huu, straika wa Namungo FC, Ibrahim Mkoko aliingia kwenye orodha ya wapiga hat-trick katika ligi hiyo wakati walipowavaa KMC na timu yake kumaliza mechi kwa ushindi wa mabao 3-1.

## Hitimana alikaribia kufukuzwa KMC FC

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya KMC imefichua kulikuwa na shinikizo kubwa la kutimua benchi lote la ufundi la timu hiyo ambalo liko chini ya Thierry Hitimana, baada ya kukosa matokeo mazuri katika mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara kwa muda mrefu.

Kauli hiyo ya KMC ilitolewa juzi baada ya timu yao kupata ushindi wa mabao 2-0 katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Kagera Sugar iliyochezwa Machi 9, mwaka huu kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam.

Ushindi huo uliifanya KMC ifikishe pointi 26 na kupanda hadi nafasi ya 12 kwenye msimamo wa ligi hiyo inayoshirikisha timu 16.

Ofisa Habari wa KMC, Christina Mwagala, alisema shinikizo hilo lilikuwa linatoka nje ya klabu yao kutokana na matokeo mabovu, lakini uongozi wa juu wa Manispaa ya Kinondoni pamoja na viongozi wengine wa timu hiyo walisimama imara kutetea.

Mwagala alisema uvumilivu wao umezaa matunda baada ya timu hiyo kuzinduka na kupata ushindi katika mechi yake iliyopita.

"Tulikuwa tunapata presha sana nje ya kambi, kila mtu alikuwa anazungumza lake. Kulikuwa na shinikizo la kuvunja benchi la ufundi, lakini viongozi wakuu kwenye manispaa walisimama imara kwa kuona bado kocha na wenzake wana uwezo wa kutuvusha hapa tulipo na kutupeleka huko mbele.

Pia wachezaji tulionao tukizidisha kuwapa morali wataenda kufanya kitu kikubwa na timu itapata matokeo chanya. Na kama ligi isingesimama, tulikuwa na nafasi nzuri ya kushinda katika mechi inayokuja," alisema Mwagala.

Aliongeza wamewapa mapumziko ya siku 10 wachezaji wao na wanatarajia kurejea tena mazoezini ifikapo Aprili 9, mwaka huu.

" Tumetoa mapumziko kwa wachezaji wetu na benchi la ufundi, hivi ninavyosema Kocha, Thierry Hitimana amekwenda kwao Rwanda kupumzika, baada ya yako tutarejea kuanza maandalizi ya kuelekea mechi yetu dhidi ya Geita Gold," alisema Mwagala.

KMC ilikuwa haijashinda mechi yoyote tangu kuingia kwa mwaka huu, kabla ya kuifunga Kagera Sugar, mara ya mwisho kupata ushindi ilikuwa ni Desemba 22, mwaka jana ilipowachapa Polisi Tanzania mabao 2-0.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### SPURS: KANE HAUZWI
KLABU ya Tottenham Hotspur haiko tayari kumuuza mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya England, Harry Kane, katika msimu wa joto hata kama mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29, ambaye mkataba wake na Spurs unakamilika msimu wa joto 2024, hatasaini mkataba mpya. ***(Sky Sports)***

### ENRIQUE AITAKA SPURS
KOCHA Mkuu wa zamani wa Timu ya Taifa ya Hispania na Barcelona, Luis Enrique, angependa kuchukua nafasi ya kuwa mwalimu mpya wa Tottenham Hotspur. ***(Times)***

### LUKAKU KUREJEA CHELSEA
OFISA Mtendaji Mkuu wa Inter Milan, Beppe Marotta, amesema mshambuliaji wa Timu ya Taifa ya Ubelgiji, Romelu Lukaku, mwenye umri wa miaka 29 atarejea Chelsea mkataba wake wa mkopo wa muda mrefu katika klabu hiyo ya Serie A utakapokamilika. ***(Sky Sport Italia)***

### ALLISTER NJIA MOJA
KIUNGO wa kati wa Timu ya Taifa ya Argentina, Alexis Mac Allister, mwenye umri wa miaka 24, anazivutia vilabu kadhaa na yuko tayari kuondoka Brighton ifikapo msimu wa joto. ***(90 Min)***

### MENDY, CHELSEA HAKIELEWEKI
GOLIKIPA wa Timu ya Taifa ya Senegal, Edouard Mendy, mwenye umri wa miaka 31 amefanya mazungumzo ya mkataba na Chelsea, lakini pande hizo mbili haziko karibu kufikia makubaliano. ***(Times)***

### UNITED KUMBANA PELLISTRI
KLABU ya Manchester United itampa kiungo wa Timu ya Taifa ya Uruguay, Facundo Pellistri, mwenye umri wa miaka 21 mkataba mpya kabla ya kumtoa kwa mkopo msimu ujao. ***(Fabrizio Romano)***

### AKHOMACH AULA LEEDS
LEEDS United imekubali kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Hispania, Ilias Akhomach, mwenye umri wa miaka 18, mwishoni mwa msimu. ***(Mundo Deportivo)***

### CITY YAMPA MITANO ALVAREZ
MSHAMBULIAJI wa Timu ya Taifa ya Argentina na Manchester City, Julian Alvarez, mwenye umri wa miaka 23, amekubali mkataba mpya wa miaka mitano na nusu na klabu hiyo ya Ligi Kuu England. ***(Football Insider)***

### TIERNEY KUBAKIA ARSENAL
KLABU ya Newcastle United inavutiwa na beki wa Arsenal, Kieran Tierney, lakini washikabunduki hao huenda wasimuuze mchezaji huyo wa kimataifa wa Scotland mwenye umri wa miaka 25 kwa sababu Kocha, Mikel Arteta, anataka kumbakisha. ***(Caught Offside)***

### LIVERPOOL, NEWCASTLE VITANI
LIVERPOOL na Newcastle zinawania kumsajili kiungo wa kati wa Timu ya Taifa ya Argentina, Alan Varela, mwenye umri wa miaka 21 kutoka Boca Juniors. ***(Football Insider)***

### LAWRENCE KUONDOKA PSG
BAADA ya miaka sita na Paris St-Germain, mchezaji wa kimataifa wa Canada, Ashley Lawrence, ameamua kutoongeza mkataba wake. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 27 ataondoka katika klabu hiyo mwishoni mwa msimu huu. ***(Le Parisien)***

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# HAALAND AFUNGA BAO LA 30 ULAYA

**Aweka rekodi mpya ya kufunga mabao mengi mapema akiwa na umri mdogo...**

**MANCHESTER, Engand**

ERLING Haaland amekuwa mchezaji mwenye umri mdogo zaidi kufikisha mabao 30 katika mashindano ya Ligi ya Mabingwa Ulaya baada ya mshambuliaji huyo wa Manchester City kufunga 'hat-trick' kipindi cha kwanza kwenye mechi dhidi ya RB Leipzig iliyochezwa juzi.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Norway alifunga mabao mawili katika muda wa dakika mbili pale kwenye Uwanja wa Etihad na kufikisha mabao 30 katika kinyang'anyiro hicho, kabla ya kuongeza goli la tatu kuelekea mapumziko.

Akiwa na umri wa miaka 22 na siku 236, Haaland alikuwa mwanaume mwenye umri mdogo kufikisha mabao hayo akimpiku nyota wa Timu ya Taifa ya Ufaransa, Kylian Mbappe.

Wachezaji wengine waliowahi kufunga idadi hiyo ya mabao wakiwa na umri mdogo ni Lionel Messi (miaka 23 na siku 131) na Raul (miaka 24 na siku 91).

Haikuwa rekodi pekee ambayo Haaland alivunja pia, bao la 30 la mshambuliaji huyo wa Ligi ya Mabingwa Ulaya lilipatikana katika mchezo wake wa 25 tu, na kuweka alama mpya kwa mechi chache zaidi zinazohitajika kufikia hatua hiyo muhimu.

Alivunja rekodi ya awali ya mechi 34, iliyokuwa ikishikiliwa na Ruud van Nistelrooy, huku mechi 46 zilimchukua Robert Lewandowski kufikia mafanikio hayo.

Haaland hakuwa amefunga bao katika mechi ya kwanza dhidi ya Leipzig iliyochezwa Ujerumani, kuelekea mechi ya Jumanne akiwa na mabao 28 ya Ligi Kuu England.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!

SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,090,5

MECHI KALI

BETIS
VERSUS
MANCHESTER UTD

1 | 3.28
X | 3.28
2 | 2.13

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.

tigo pesa
vodacom | m-pesa
halopesa
airtel money

SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#

GBT:0249 18+
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588

@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# MUSTAKABALI WA LUKAKU HAUNA UHAKIKA



**MILAN, Italia**

MUSTAKABALI wa Romelu Lukaku umegubikwa na sintofahamu baada ya Mkurugenzi wa Inter Milan, Beppe Marotta, kukiri mshambuliaji huyo "bado hajawa sawa" kufuatia kipindi kigumu cha pili akiwa na Nerazzurri hao.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ubelgiji alifurahia kucheza kwa mara ya kwanza akiwa na Inter kati ya 2019 na 2021, akifunga mabao 64 katika mechi 95 na kuwasaidia kushinda taji la Ligi Kuu.

Hata hivyo, amefunga mabao matano pekee kwa kikosi hicho cha Simone Inzaghi, tangu arejee kutoka Chelsea kwa mkopo wa msimu mzima tangu Juni mwaka jana.

Ingawa, mabao matatu kati ya hayo yamepatikana katika mechi zake tano zilizopita, ikiwa ni pamoja na ushindi wa dakika za lala salama katika mechi ya kwanza ya hatua ya 16 bora ya Ligi ya Mabingwa Ulaya dhidi ya Porto.

Inaonekana iwapo mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 ataongeza muda wake wa kusalia hapo San Siro au atarejea Chelsea baada ya kumalizika kwa muda wake wa mkopo.

Lakini Marotta alionekana kutokubali, akiamini Inter bado hawajaona ubora wa Lukaku, ambaye anahisi pia aliathiriwa na bidii yake wakati wa Kombe la Dunia nchini Qatar.

"Hayuko fiti kwa asilimia 100, bado sio Lukaku yule tuliyemwona miaka ya nyuma."

# Morocco kuandaa Kombe la Dunia

**RABAT, Morocco**

TAIFA la Afrika Kaskazini, Morocco litaungana na Hispania na Ureno katika jitihada za nchi tatu za kuandaa fainali za Kombe la Dunia zitakazofanyika mwaka 2030, maofisa walithibitisha Jumanne.

Hispania na Ureno hapo awali ziliungana na Ukraine kama mshirika wa uwezekano wa kuandaa michuano hiyo ya mwaka 2030, lakini kutokana na vita inayoonekana kutokuwa na mwisho huko Urusi, Waarabu wa Morocco wameingia kuchukua nafasi hiyo.

"Ningependa kutangaza Ufalme wa Morocco umeamua, pamoja na Hispania na Ureno, kuwasilisha ombi la pamoja la kuandaa Kombe la Dunia la 2030," Mfalme wa Morocco Mohammed VI alisema katika barua iliyosomwa na Waziri wa Michezo wa nchi hiyo, Chakib Benmoussa, mjini Kigali, katika Kongamano la 73 la Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), litakalofanyika leo.

"Zabuni hii ya pamoja, ambayo haijawahi kutokea katika historia ya soka, italeta pamoja Afrika na Ulaya.

"Pia italeta yaliyo bora zaidi kwetu sote, kwa hakika mchanganyiko wa fikra, ubunifu, uzoefu na mbinu."



Morocco imejitosa katika fainali kadhaa za Kombe la Dunia huko nyuma, ikikaribia zaidi katika mbio za kuandaa mwaka 2010 ambapo walishindwa na Afrika Kusini.

583,531/-

# MAYELE KAMILI KUIVAA US MONASTIR JUMAPILI

Na **Saada Akida**

HABARI njema kwa mashabiki wa Yanga ni kurejea mazoezini kwa mshambuliaji wao nyota, Fiston Mayele (pichani), ambaye alikuwa majeruhi, imefahamika.

Mayele jana aliungana na wachezaji wengine wa timu hiyo kwa ajili ya maandalizi ya mchezo wa mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Monastir kutoka Tunisia.

Mkongomani huyo alipata majeraha madogo katika mechi dhidi ya Real Bamako na kusababisha kutocheza mchezo wa Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Geita Gold FC uliopigwa kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam juzi.

Akizungumza na gazeti hili jana, Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, alisema Mayele anaendelea vizuri na wanaamini atakuwa tayari kuwavaa US Monastir.

Kaze alisema nyota huyo hakupata majeraha makubwa na amerejea kikosini kuongeza nguvu za kusaka pointi tatu muhimu dhidi ya US Monastir ili wasonge mbele katika mashindano hayo.

"Mayele alishauriwa kupumzika kidogo, tukampuzisha katika mchezo dhidi ya Geita Gold FC na leo (jana) jioni amerejea uwanjani ili kuendelea kujiimarisha kuelekea mchezo wetu wa Jumapili dhidi ya US Monastir," alisema Kaze.

Aliongeza kwa sasa kazi kubwa ya benchi la ufundi la timu hiyo ni kuhakikisha safu ya ushambuliaji inakuwa makini zaidi kutumia vizuri nafasi wanazotengeneza hasa dakika za mwanzo za mchezo.

"Kazi kubwa tunayoifanya ni kujenga stamina za wachezaji, katika mazoezi ya Gym asubuhi na jioni tunawaimarisha, kiufundi tunaanza mbinu zitakazotubeba huku tukiyarekebisha makosa tuliyofanya kwenye mechi zilizopita," Kaze aliongeza.




# Simba, Yanga zakimbiana FA

INATOKA UK. 24

zuri kwa sababu tunamhitaji mshindi wa kwanza wa robo fainali kati ya Simba dhidi ya Ihefu FC, kwa upande wetu tunamhitaji sana Simba," alisema Ibwe.

Naye Katibu Mkuu wa Chama cha Mpira wa Miguu Mkoa wa Dar es Salaam (DRFA), Ramadhani Misiru, amewapongeza TFF na Azam Media kwa kuendelea kuboresha droo ya michuano hiyo ambayo hufanyika kwa uwazi na weledi.

"Mkoani (Dar es Salaam), kwetu tuna mechi tatu, tunakaribisha wageni wetu, tunaamini mechi zitakuwa nzuri na timu zetu zina uhakika wa kufanya vizuri," alisema Misiru.

Bingwa wa michuano hiyo hupata tiketi ya kuiwakilisha Tanzania Bara kwenye michuano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika ambayo hufanyika kila mwaka.


# SUPA JACKPOT
# MECHI WIKI HII
## BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01.18/03/23 | 18:00 | Aberdeen FC vs Heart of Midlothian FC | 2.38 | 3.40 | 2.65 |
| 02.18/03/23 | 18:00 | Rotherham United vs Cardiff City | 2.55 | 3.15 | 2.65 |
| 03.18/03/23 | 18:00 | Stoke City vs Norwich City | 2.65 | 3.15 | 2.55 |
| 04.18/03/23 | 18:15 | Albacete Balompie vs Granada CF | 2.55 | 2.95 | 2.80 |
| 05.18/03/23 | 18:30 | Portimonense SC vs FC Vizela | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 06.18/03/23 | 20:30 | Espanyol Barcelona vs RC Celta de Vigo | 2.75 | 3.05 | 2.50 |
| 07.18/03/23 | 20:45 | FC Emmen vs Sparta Rotterdam | 2.50 | 3.10 | 2.70 |
| 08.18/03/23 | 21:00 | Quevilly-Rouen Metropole vs FC Metz | 2.60 | 2.95 | 2.75 |
| 09.18/03/23 | 21:00 | Chamois Niort FC vs Stade Lavallois MFC | 2.60 | 3.00 | 2.70 |
| 10.19/03/23 | 14:15 | FC Groningen vs SC Heerenveen | 2.70 | 3.20 | 2.46 |
| 11.19/03/23 | 14:30 | Sampdoria Genoa vs Hellas Verona | 2.85 | 3.00 | 2.48 |
| 12.19/03/23 | 15:30 | Eintracht Braunschweig vs Hannover 96 | 2.46 | 3.30 | 2.65 |
| 13.19/03/23 | 16:30 | Excelsior Rotterdam vs SC Cambuur | 2.55 | 3.30 | 2.50 |
| 14.19/03/23 | 17:00 | ESTAC Troyes vs Stade Brest 29 | 2.70 | 3.20 | 2.45 |
| 15.19/03/23 | 18:15 | CA Osasuna vs Villarreal CF | 2.90 | 3.05 | 2.40 |
| 16.19/03/23 | 19:00 | FK Austria Wien vs SK Rapid Wien | 2.40 | 3.15 | 2.45 |
| 17.19/03/23 | 20:00 | Lazio Rome vs AS Roma | 2.60 | 2.95 | 2.75 |

# MECHI ZA USHINDI

"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

## ALHAMISI - 16/03/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 13:00 | 4323 | Bali Utd Pusam vs Persepam MU | 1.82 | 3.49 | 3.65 |
| 14:00 | 3931 | Lernayin Artsakh vs Pyunik Yerevan | 8.51 | 4.36 | 1.33 |
| 14:30 | 1363 | Shahrdari Hamedan vs Khosheh Talaei | 2.25 | 2.55 | 3.30 |
| 14:30 | 1855 | Shahrdari Astara vs Arman Gohar Sirjan | 2.70 | 2.59 | 2.91 |
| 14:30 | 3222 | Saipa Karadj vs Shams Azar Qazvin | 3.99 | 2.85 | 2.01 |
| 14:30 | 3551 | Vanpars vs Chador Malu Yazd | 2.15 | 2.60 | 3.45 |
| 14:30 | 4832 | Caspian Babol vs Esteghlal Mollasani | 2.11 | 2.69 | 3.93 |
| 14:30 | 5152 | Kheybar Khorramabad FC vs Khalijfars Mahshahr | 1.50 | 3.52 | 6.63 |
| 15:00 | 4768 | CA Tigre Reserve vs Arsenal FC Reserve | 2.04 | 3.11 | 3.47 |
| 15:00 | 5601 | Banfield Reserve vs CA Talleres de Cordoba Reserve | 2.28 | 2.95 | 3.11 |
| 15:15 | 2870 | Negeri Sembilan vs Terengganu | 3.30 | 3.20 | 1.91 |
| 16:00 | 3832 | FK Zlatibor vs FK Graficar Beograd | 4.53 | 3.50 | 1.66 |
| 16:00 | 4817 | Al Khaleej Club vs AL Tai | 2.75 | 3.10 | 2.20 |
| 16:30 | 2453 | Fidelis Andria vs Crotone | 4.67 | 3.24 | 1.83 |
| 17:00 | 1516 | Bkma Yerevan vs Urartu | 10.40 | 4.37 | 1.29 |
| 17:00 | 5394 | Tabor Sezana vs ND Gorica | 2.53 | 3.01 | 2.61 |
| 18:00 | 1328 | Neftchi Baku vs Kapaz | 1.36 | 4.35 | 7.46 |
| 18:00 | 3441 | Nizhny Novgorod vs Rostov | 2.52 | 3.06 | 2.65 |
| 18:30 | 1054 | Etehad Alreef vs Bouri | 5.19 | 3.89 | 1.54 |
| 18:30 | 2440 | AL Ittihad Bhr vs Busaiteen | 2.90 | 3.26 | 2.23 |
| 18:30 | 5368 | Najma Manama vs Um Alhassam | 1.42 | 4.27 | 6.25 |
| 18:30 | 5828 | Aali vs Qalali | 2.25 | 3.21 | 2.90 |
| 19:00 | 1103 | Hapoel Beer Sheva W vs Maccabi Bnot Emek Hefer W | 2.55 | 3.85 | 2.05 |
| 19:00 | 2066 | Parnu JK Vaprus vs Nomme Kalju | 10.17 | 5.61 | 1.21 |
| 19:00 | 4219 | CSA Steaua Bucuresti vs Unirea Dej | 1.70 | 3.44 | 4.31 |
| 19:30 | 1343 | Catanzaro vs Nuova Monterosi | 1.26 | 5.32 | 11.70 |
| 19:30 | 3866 | NK Mura vs Luka Koper | 2.29 | 3.02 | 2.92 |
| 20:00 | 2570 | Doxa Katokopia vs Karmiotissa | 2.03 | 3.33 | 3.49 |
| 20:45 | 1660 | Feyenoord vs Shakhtar Donetsk | 1.47 | 4.24 | 6.05 |
| 20:45 | 1802 | Slovan Bratislava vs FC Basel | 2.45 | 3.22 | 2.77 |
| 20:45 | 2545 | Fenerbahce vs Sevilla FC | 2.28 | 3.39 | 2.89 |
| 20:45 | 2594 | Hapoel Nir Ramat Hasharon W vs Maccabi Kishronot Hadera W | 2.55 | 3.85 | 2.05 |
| 20:45 | 3443 | Djurgardens IF vs Lech Poznan | 2.47 | 3.23 | 2.73 |
| 20:45 | 3516 | Betis vs Manchester Utd | 3.28 | 3.28 | 2.13 |
| 20:45 | 4486 | SC Freiburg vs Juventus | 2.91 | 3.06 | 2.44 |
| 20:45 | 5550 | Sivasspor vs Fiorentina | 4.74 | 3.83 | 1.64 |
| 21:00 | 4585 | Fortaleza CE U20 vs Atletico PR U20 | 3.10 | 3.30 | 2.11 |
| 21:00 | 5947 | MS Kiryat Gat W vs AS Tel Aviv University W | 1.06 | 8.20 | 14.00 |
| 21:30 | 4055 | Hapoel Katamon Jerusalem W vs Hapoel Petach-Tikva W | 1.49 | 4.46 | 4.87 |
| 22:00 | 1478 | QPR U23 vs Charlton U23 | 2.06 | 3.69 | 2.91 |
| 22:00 | 5626 | Sepsi Osk vs U Craiova SA | 1.89 | 3.19 | 4.03 |
| 22:45 | 1192 | Drogheda Utd vs Dundalk FC | 3.33 | 3.18 | 2.02 |
| 23:00 | 1325 | Real Sociedad vs Roma | 2.13 | 3.14 | 3.44 |
| 23:00 | 1457 | Villarreal vs Anderlecht | 1.44 | 4.33 | 6.45 |
| 23:00 | 1538 | Arsenal vs Sporting Lisbon | 1.39 | 4.51 | 7.14 |
| 23:00 | 2346 | AZ Alkmaar vs Lazio | 2.83 | 3.23 | 2.40 |
| 23:00 | 2791 | Nice vs Sheriff Tiraspol | 1.42 | 4.34 | 6.86 |
| 23:00 | 3704 | Union Saint Gilloise vs Union Berlin | 3.03 | 3.18 | 2.30 |
| 23:00 | 5482 | Ferencvaros TC vs Bayer Leverkusen | 3.43 | 3.48 | 2.00 |
| 23:00 | 5977 | West Ham vs AEK Larnaca | 1.24 | 5.45 | 11.09 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo

Alhamisi Machi 16, 2023

Nipashe



UKURASA 21

# Haaland afunga bao la 30 Ulaya



Ofisa Habari wa Yanga, Ali Kamwe (katikati), akiwa na shabiki wa klabu hiyo wa eneo la Manzese (jina halikupatikana), Dar es Salaam ambaye alipata nafasi ya kuzungumza na wachezaji wa timu yao kama sehemu ya hamasa kuelekea mechi ya Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Monastir ya Tunisia itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam. **PICHA: MTANDAO**

## Stars kwenda kujichimbia Misri

**Na Hadija Mngwai**

KIKOSI cha Timu ya Soka ya Taifa (Taifa Stars), kitaondoka nchini kwa makundi kuelekea Misri kwa ajili ya kuweka kambi maalumu ya kujiandaa kuwakabili Uganda (Cranes), katika mechi ya kwanza ya kusaka tiketi ya kushiriki michuano ya Afrika (AFCON), imefahamika.

Uganda itawaalika Taifa Stars Machi 24, mwaka huu katika mji wa Ismailia, Misri na timu hizo zitarudiana Machi 28, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

Ofisa Habari wa TFF, Clliford Ndimbo, alisema jana kikosi cha Stars kitasafiri kwa awamu mbili na hiyo imetokana na timu za Simba na Yanga kukabiliwa na mechi za mashindano ya CAF.

"Kikosi cha Stars kinatarajia kuondoka katika makundi mawili kuelekea Misri, kundi la kwanza litaondoka Machi 16 na la pili Machi 20, kwenda kuweka kambi huko Misri, tumefanya hivyo kwa sababu kuna timu zinakabiliwa na mashindano ya CAF, kwa maana ya Simba na Yanga.

Tunatazama mchezo huu kwa umakini mkubwa, nia ni kuona tunafanikiwa kuingia katika mashindano ya AFCON 2023, kwa mara ya tatu, ndio maana tunahakikisha kila kitu kinakaa sawa," alisema Ndimbo.

Aliongeza benchi la ufundi limejipanga kuhakikisha wanafikia malengo ya kufuzu fainali hizo za AFCON kwa mara nyingine.

Mara ya mwisho Taifa Stars ilishiriki fainali za AFCON mwaka 2019, ambazo zilifanyika Misri, iliongozwa na Mnigeria, Emmanuel Amunike.

# SIMBA, YANGA ZAKIMBIANA FA

### ●●● Kila upande watamba kufanya vizuri katika michuano hiyo ili...

**Na Saada Akida**

MABINGWA watetezi wa mashindano ya Kombe la FA, Yanga itakutana na Geita Gold FC ya Geita katika mechi ya hatua ya robo fainali ya michuano hiyo wakati Wekundu wa Msimbazi, Simba wao watawakaribisha Ihefu SC kutoka Mbarali, Mbeya imefahamika.

Mechi hizo za robo fainali zimepangwa kuchezwa kati ya Aprili Mosi na 6, mwaka huu.

Yanga itawakaribisha kwa mara nyingine Geita Gold FC kwenye Uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam wakati Simba itaendelea kutumia dimba la Uhuru.

Mechi nyingine za robo fainali zitakuwa ni kati ya Azam FC dhidi ya Mtibwa Sugar itakayochezwa kwenye Uwanja wa Azam Complex na Singida Big Stars watakuwa nyumbani kwenye Uwanja wa CCM Liti kuwaalika Mbeya City.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Mashindano ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), Baraka Kizuguto, alisema mechi ya hatua ya nusu fainali ya kwanza itapigwa kati ya mshindi wa mchezo kati ya Simba na Ihefu dhidi ya mshindi wa mechi ya Mtibwa na Azam wakati nusu fainali ya pili itamkutanisha mshindi wa mchezo kati ya Yanga na Geita Gold FC dhidi ya Singida Big Stars na Mbeya City.

Kizuguto alisema tarehe za michezo hiyo zimepangwa kwa kuzingatia ratiba ya Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na ushiriki wa timu za hapa nyumbani katika mashindano ya kimataifa.

"Tunatarajia kutumia viwanja viwili katika hatua ya nusu fainali, mchezo wa nusu fainali ya kwanza utachezwa kwenye Uwanja wa Nangwanda Sijaona ulioko Mtwara na nusu fainali ya pili utachezwa CCM Liti na fainali itafanyika kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga," alisema Kizuguto.

"Tunawakumbua wenyeji kuendelea kuboresha viwanja, endapo kiwanja hakitakidhi mahitaji, hatutasita kupeleka mashindano sehemu nyingine," Kizuguto aliongeza.

Mkurugenzi wa Wanachama wa Simba, Hamisi Kisiwa, alisema wamepokea vizuri droo hiyo na wanawaheshimu Ihefu kwa sababu ni timu nzuri, hivyo watajiandaa vyema kuwakabili ili kuvuka hatua hiyo ya kucheza nusu fainali.

"Tunaenda kucheza na Ihefu FC kwa tahadhari kubwa na tutawakomboa ndugu zetu waliopo kifungoni kwa mpinzani wetu huyo ambaye kuna wenzetu walishindwa kupata matokeo mazuri," alisema Kisiwa.

Naye Mratibu wa Yanga, Hafidh Saleh, alisema Yanga itaendelea kujiimarisha ili kuhakikisha wanafanya vizuri katika mbio za kutetea taji hilo.

"Geita Gold FC tulikutana nao katika ligi mara mbili na zote tumewafunga, sasa tunaenda kujiandaa vyema kuwakaribisha tena kupata kichapo na kucheza nusu fainali ya ASFC, ili kufikia malengo yetu ya kucheza nusu na fainali," alisema Saleh.

Ibrahim Mohammed, Mratibu wa Singida Big Stars, alisema kuelekea mchezo huo dhidi ya Mbeya City, wamejiandaa vyema kutumia uwanja wa nyumbani kwa kupambana na kusaka nafasi ya kucheza nusu fainali.

Ofisa Habari wa Azam FC, Hashim Ibwe, alisema malengo yao makubwa ni kufanya vizuri katika mchezo dhidi ya Mtibwa Sugar ili wasonge mbele na kukaribia malengo yao.

"Mtibwa Sugar inatakiwa kujipanga vi-

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >